




UKURASA 3

## SILAA ataka mfumo mmoja kielektroniki




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Mei 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580952

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com


www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Ngono ya mdomo kichaka cha VVU



UKURASA 2






1

**SALOME MAKAMBA**
"Hii ninahesabu kama ni hujuma kwa Watanzania kama ndiyo wanavyofanya basi Mheshimiwa Waziri haujatenda haki."

2

**ANTIPUS MGUNGUSI**
"Nilipoteza simu lakini hadi sasa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) wanaitafuta kwa sababu walinimbia hawawezi kuipata mpaka iwashwe."

3

**NEEMA LUGANGIRA**
"Bado kuna tatizo la mitandao katika mikoa mingi iliyo pembezoni mwa nchi kama Mwanza na Kigoma. Wananchi walalalamika kutokupata mawasiliano kwa wakati."

**IDDI KASSIM IDDI**
"Kumekuwa na wizi wa bando. Mtu anajibana ili atumie siku 30 lakini hajui zimeishia wapi. Hizi dakika na mabando tunazoibiwa zinakwenda wapi?"

**NAPE NNAUYE**
"Bando ni huduma ya ziada kwenye huduma za data. Mtoa huduma anaamua kutengeneza bando nyingi ili akupe wigo wa uchaguzi wa huduma unayotumia."



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

## Waziri agoma kutoa msamaha wa kodi kwa gari la kifahari Zenj

UKURASA 3

# Wabunge wacharuka ukomo matumizi vifurushi intaneti

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YAPANGUA KIKOSI CHA YANGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Ngono ya mdomo kichaka cha VVU

**Na Sanula Athanas,**
MOROGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya DARE, Dk. Lillian Benjamin, ameitaka jamii kuacha ngono ya mdomo kwa kuwa ni hatari kiafya, hasa kusababisha maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Amesema ute unaopatikana chini ya fizi na maji yaliyopo kwenye sehemu za siri za mwanamke, yamethibitika kitaalamu kuwa na VVU, hivyo kufanya ngono kwa mdomo kunaongeza uwezekano wa kuambukizwa virusi hivyo.

Akiwasilisha mada kuhusu uelewa wa VVU/UKIMWI wakati wa semina kwa wahariri na waandishi wa habari mjini Morogoro jana, Dk. Lillian alisema aina hiyo ya mapenzi ni hatari kwa kuwa mbali na kuchochea maambukizo ya VVU, wahusika wako hatarini kupata maradhi mengine.

"Ninashauri jamii iachane na aina hii ya ngono kwa sababu ni hatari kwa afya yao," Dk. Lillian alisema.

Nyangusi Laiser, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), akizungumzia suala hilo, alisema: "Ngono ya mdomoni ni hatari kwa kuwa maji maji yaliyoko mdomoni yanaweza kuwa na chembe chembe za damu ikiwa mdomoni kuna michubuko, hivyo kama mtu ameambukizwa VVU, anaweza kumwambukiza mwenza wake VVU.

"Ikiwa ngono inahusisha mdomo kwenye via vya uzazi, kuna hatari ya kuambukizwa kupitia maji maji ya sehemu za siri za mwanamke," ofisa huyo alionya.

Akirejea takwimu za kitaifa na kimataifa, Laiser alibainisha kuwa kwa mwaka 2020, kulikuwa na watu milioni 37.7 waliokuwa wanaishi na VVU duniani.

Kati yao, watoto wenye umri chini ya miaka 15 ni milioni 1.7 na kwamba asilimia 53 ya waliokuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi walikuwa wanawake.

Laiser alisema maambukizo mapya kwa mwaka 2020 yalikuwa watu milioni 1.5, kukionekana kuwapo kupungua kutoka watu milioni tatu mwaka 1997.

"Takwimu zinaonyesha kila siku takriban watu 4,000 huambukizwa VVU duniani na kati yao, 2,400 (asilimia 60) ni waliopo kusini mwa Jangwa la Sahara," alibainisha. Kwa Tanzania, ofisa huyo alisema kuwa kwa mwaka 2020, watu waliokuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi walikuwa milioni 1.7.

"Maambukizo mapya mwaka 2020 nchini yalikuwa watu 68,000. Kati yao, 37,000 ni wanawake, wanaume 21,000 na watoto wenye umri chini ya miaka 15 wapatao 10,000.

Vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 wanaongoza kwa maambukizo mapya wakiwa asilimia 80," alibainisha.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango (wa pili kulia), akikabidhi cheti cha shukrani ya kudhamini wiki ya maonesho ya kitaifa ya ubunifu (MAKISATU), kwa Mkuu wa Idara ya ubunifu wa Benki ya NMB, Jossina Njambi, katika hafla ya kufunga maonyesho hayo jijini Dodoma jana. Wengine ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia) na Mkuu wa Idara ya huduma za Serikali wa Benki hiyo, Vicky Bishubo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge wacharuka ukomo matumizi ya vifurushi intaneti

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

BAADHI ya wabunge jana walitoa kilio chao kuhusiana na suala zima la kumalizika haraka kwa matumizi ya kifurushi cha intaneti (bando), huku wakiishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa mfumo wa kifurishi cha intaneti kuisha kama zilivyo nchi nyingine.

Pia wameiomba serikali katika kipindi hiki cha kuendelea Tanzania ya kidijitali, kuhakikisha mawasiliano yanapatikana nchi nzima ikiwamo maeneo ya pembezoni. Waliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba alisema Mei 13, mwaka jana, aliuliza swali lililohusu vifurushi vya mtandao ambavyo havijatumika, Waziri alisema alielekeza kampuni za simu endapo mtu kama bando lake limekwisha muda wake na akinunua lingine ule muda uliopita harudishiwi.

"Hii ninahesabu kama ni hujuma kwa Watanzania kama ndiyo wanavyofanya basi Mheshimiwa Waziri (Nape) haujatenda haki," alisema Makamba.

Akiendelea kuchangia Salome alisema Watanzania asilimia 95 wanapata mtandao na wanaweza kujiunga kupiga simu, kwamba asilimia 68 wanauwezo wa kujiunga kwenye vifurushi vya mtandao.

Alisema mtumiaji wa simu akijiunga kifurushi cha intaneti cha siku moja anapaswa atumie ndani ya muda husika, kwamba endapo akishindwa kutumia kifurushi alichojiunga ndani ya muda huo kutokana na matatizo ya mtandao hawezi kurudishiwa gharama zake alizotumia.

Alisema kampuni za simu zikifanikiwa kupata Sh. 200 tu Kwa Watanzania milioni 50 kwa siku wanaweza kukusanya Sh. bilioni 10 na kwa mwezi zaidi ya Sh. bilioni 300.

"Mheshimiwa Waziri ameomba fedha kwa ajili ya wizara yake Sh. bilioni 282, kwa fedha hii yanaweza (kampuni) zinaweza kukusanya ndani ya mwezi mmoja tu. Sasa kusema hiyo ni biashara ni nguvu ya mazungumzo na kazi ya wizara ni kuwalinda Watanzania.

"Biashara ya kifurushi cha intaneti kuisha duniani imepitwa na wakati, nchi zilizoendelea hakuna bando kuisha muda. Kwa nini turuhusu kampuni za simu ziibe fedha za Watanzania?."

Mbunge wa Malinyi, Antipus Mgungusi, alisema alipoteza simu lakini hadi sasa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) wanaitafuta kwa sababu walimwambia hawawezi kuipata mpaka iwashwe.

Mbunge wa Msalala (CCM), Iddi Kassim Iddi alisema: "Kumekuwa na wizi wa bando mtu anajibana ili atumie siku 30 lakini hajui zimeishia wapi. Hizi dakika na mabando tunazoibiwa zinakwenda wapi? Mh. Waziri Nape uje na majibu"

**ALICHOSEMA NAPE**

Waziri Nape alisema: "Jambo hilo tutalizungumza wakati wa semina ya wabunge kabla ya bunge kumalizika. Bando ni huduma ya ziada kwenye huduma za data, mtoa huduma anaamua kutengeneza bando nyingi ili akupe wigo wa uchaguzi wa huduma unayotumia."Alisema hapa nchini asilimia 97 ya watumiaji wa data wanatumia ya ziada, majirani (nchi jirani) wanatumia basic tarrif kwa sababu bando ni sehemu ndogo.

Alisema data moja inazalishwa kwa Sh. 2.3 mpaka Sh. tisa, Tanzania tunazalisha kwa Sh. 1.5 ambayo ni chini ya kuzalisha, watoa huduma wakaamua kuweka bando nyingi ili kutoa fursa kwa kila mtu anachokihitaji.

Nape alisema: "Ni sawasawa na ukipewa tiketi ya basi ya mwezi mmoja ikiisha huwezi kwenda kudai kama unavyodai kwenye mitandao ya simu. Hiyo tiketi unapewa kama ofa. Hapa kuna maneno yanasemwa kuna wizi wizi wizi, tumefanya utafiti mwingi wa kutosha na tukatoa wito kama kuna mtu ameibiwa njooni tufanye uchunguzi."

## Nape: Bil.283/- kuleta mapinduzi ya kiuchumi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema bajeti ya wizara hiyo ya Sh. bilioni 282.5 katika mwaka wa fedha 2022/23, imelenga kuleta mapinduzi ya kiuchumi kupitia utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

Akiwasilisha jana bungeni jijini Dodoma makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, Waziri Nape alisema mradi huo unalenga kuleta mabadiliko ya kidijitali kwa kuwezesha muunganisho wa kijiditali ya kikanda na kimataifa ili kukuza uchumi katika eneo hilo.

Alisema wizara yake inasimamia mapinduzi hayo na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari nchini.

"Mapinduzi ya kidijitali ndiyo yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano," alisema.

Alisema wizara imepanga kufanya mabadiliko na maboresho kwenye sekta ili kuendana na mageuzi kwa kuharakisha uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya TEHAMA, mawasiliano, posta na habari anwani za makazi, mitambo ya utangazaji na posta.

Nape alisema mapinduzi hayo yanawezeshwa na misingi muhimu ikiwamo TEHAMA, mifumo ya mawasiliano, tendaji, fedha, usambazaji kwa njia ya posta, uwapo wa vyombo vya upashanaji habari pamoja na uimara wa uhuru husika.

Aidha, alisema uchumi wa kidigitali unawekewa mazingira bora ya kiudhibiti, kiuwekezaji na matumizi kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa kampuni changa.

Alisema matokeo ya mradi huo ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo na kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya serikali na waliopo nje ya Serikali.

Matokeo mengine ni kuongeza uwezo wa utoaji wa huduma za serikali kwa kuwezesha uwapo wa intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya serikali ili kumnufaisha mwananchi.

Nape alisema katika mwaka 2022/23, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Sh. bilioni 39.3 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kujenga kituo kimoja cha kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitano kwenye kila Kanda.

Alisema fedha hizo zitawezesha ununuzi, ugavi na ufungaji wa vifaa katika kituo kimoja kikubwa na vituo vidogo vitano vya kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na kuwezesha ununuzi wa 'bandwidth' kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya serikali.

Alisema pia watafanya mapitio na kuhuisha sera, sheria na kanuni mbalimbali za TEHAMA, kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia wataalamu 200 mafunzo ya muda mfupi na wataalamu 10 mafunzo ya muda mrefu na kufanya tathmini ya kuainisha mahitaji na usanifu wa kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

**ANWANI ZA MAKAZI**

Kuhusu anwani za makazi, Nape alisema hadi Aprili mwaka huu jumla ya anwani za makazi 12,171,320 zimekusanywa na kuingizwa kwenye programu tumizi.

**MKONGO WA TAIFA**

Alisema hadi Aprili mwaka huu wamekamilisha taratibu za manunuzi za kuwezesha ujenzi wa kilomita 4,442 kutoka kiwango cha 200G hadi 800G na kujenga vituo 37, upanuzi wa vituo 75 vya kutoa huduma ambavyo mikataba 22 ya Sh. bilioni 141 imesainiwa.

## Mbunge atishia kuondoka na Siwa

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Mbinga Vijijini (CCM), Benaya Kapinga, ametishia kuondoka na Siwa ya Bunge endapo fedha za barabara jimboni kwake zilizochukuliwa kwa ajili ya mchakato wa anuani za makazi hazitarejeshwa.

Alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya mwaka wa fedha 2022/23.

Mbunge huyo alisema katika Wilaya ya Mbinga mchakato wa anuani za makazi umefanyika vizuri lakini wanashida ya barabara hali iliyosababishwa na fedha zilizotengwa awali kuelekezwa kwenye mchakato wa anwani za makazi.

Alisema barabara hizo zinahudumia wananchi wa kata nne ambao kwa sasa wanalazimika kwenda umbali wa kilometa 30 kufuata huduma ya hospitali.

Kapinga alisema hafahamu kama maeneo mengine kumefanyika kama ilivyofanyika Mbinga na kuhoji kama hayajafanyika kwa nini wao wamefanyiwa kwa barabara zinazokwenda kwenye hospitali.

"Hivi kati ya barabara na mabao kipi ni muhimu zaidi?, hivi ni nani anaweza kuvumilia kukosa kibao na kukosa kupita njia nzuri kwenda hospitali?, barabara hii inapitiwa na kata nne hali ya barabara hizi ni mbaya sana.," alihoji.

Akiendelea kuchangia mbunge Kapinga alisema hajaukataa mradi wa anwani za makazi.

"Nilikuwa nahoji hivi mtu akikosa kusoma kibao na kukosa barabara yupi ataumia hapo? Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi, barabara hii mwaka 2020/21 iliombewa fedha tukatenga ikaondolewa na mwaka 2021/22 tulitengewa, imeondolewa tena.

"Kwa sababu zipi za msingi nilikuwa nahoji. Hivi ilivyofanyika Mbinga ndivyo ilivyofanyika majimbo mengine kama sivyo kwa nini sisi tufanyiwe hivyo," alisema.

Alisema barabara hizo zinakwenda kwenye hospitali ya Mbinga na wananchi wanazitumia.

"Barabara hizi zina mashimo, mawe haipitiki sasa hivi wananchi wanalazimika kwenda Mbinga kilometa zaidi ya 30 wakati hapo ni kilometa 10 tu. "Mama mjamzito anaongezewa safari zaidi ya kilometa 10 jambo hili limenisikitisha sana pamoja na uzuri wa mradi huu pamoja ninaheshimiana na Mheshimiwa Nape ninataka kwenye majumuisho aeleze fedha hizi zitarejeshwaje na miradi hii itatekelezwaje. Bila hivi nitaondoka na Siwa hii haiwezekani hili Siwa nitatoka nalo, lazima aniambie Mheshimiwa Nape." alisisitiza.

Baada ya kauli hiyo, Waziri wa Nchi-Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), George Simbachawene alisema: "Mheshimiwa Mbunge ninamheshimu sana na ni bado kijana na ni mbunge wa mara ya kwanza kwenye rekodi zetu hakuna mtu amewahi kuondoka na Siwa.

"Utakuwa mbunge wa kwanza, hii Siwa ndiyo Bunge lenyewe kwa mujibu wa utaratibu wa mabunge ya Jumuiya ya Madola Siwa ndiyo heshima yetu ndiyo tunalolisalimia hapo ndiyo inayoshika mamlaka ya Spika

"Ukiondoka na hili siwa maana yake umeondoka na Bunge lote umekwenda nalo Mbinga nikuombe ama ufute maneno hayo ili uendeee kutoa mchango wako mzuri, ninaamini wewe ni mbunge mzuri,"

Baada ya maelezo hayo Mbunge Kapinga alifuta maneno hayo aliyotamka awali.

# Waziri agoma msamaha kodi kwa gari la kifahari

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Zanzibar Fedha na Mipango, Saada Mkuya Salum, amesema wizara imekataa kutoa msamaha wa kodi ya Sh. milioni 308.5 kwa gari la kifahari aina ya Benzi.

Gari hilo ni la Kampuni ya Turkys Mifuko inayomilikiwa na mfanyabiashara Toufky Salum Turky na kwamba maombi ya msamaha huo yalikuwa kinyume cha Sheria ya Uwekezaji.

Akizungumza na waandishi wa babari ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar, Waziri Saada alisema msamaha wa kodi kwa wawekezaji unapaswa kutolewa wakati wa ujenzi wa mradi na siyo baada ya mradi kukamilika na kuanza kuzalisha. "Kwa mujibu wa kumbukumbu zetu, maombi yake ya msamaha wa kodi kwa Kampuni ya Mifuko Turky yalikataliwa na waziri kwa sababu yameletwa kinyume na sharia, mradi ukiwa tayari umeanza uzalishaji kinyume na sheria.,"alisema Waziri Saada.

Alisema kwa mujibu wa sharia, mwekezaji anaweza kunufaika na msamaha wa kodi wakati wa ujenzi wa mradi, lakini baada ya mradi kukamilika na kuanza uzalishaji, fursa ya msamaha wa kodi inakuwa imemalizika.

Alisema kwa msingi huo, ndiyo maana Wizara iliamua kuyatupa maombi ya kampuni hiyo ya kutaka msamaha wa kodi. "Wizara kazi yetu kubwa kusimamia sheria, taratibu na mifumo hatuwezi kufanya mambo kinyume cha sheria hasa katika suala la kusimamia mapato ya serikali," alisisitiza.

Naibu Kamishina wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar, Juma Hasssan Hassan, alisema baada ya maombi yao wanatakiwa kurudi TRA kulipa kiwango hicho cha kodi.

Alisema TRA inaendelea kuwafuatilia kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za kusimamia sheria ili kuhakikisha fedha hizo zinalipwa baada ya waziri kukataa kutoa msamaha wa kodi wa gari hilo la kifahari.

Kaimu Meneja Uhusiano na Elimu kwa Walipakodi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Makame Khamis Mohamed, alisema gari hilo limesajiliwa na kupewa namba Z-1 kutokana na wahusika kulipa Sh. milioni 15 baada ya kuingizwa Januari, mwaka huu.

Alisema kama gari linatembea mitaani, watakuwa wanavunja sheria kwa sababu hairuhusiwi kutembea kabla ya kukamilisha malipo ya kodi.




Baadhi ya wananchi wa Mji wa Geita, wakijipatia mahitaji katika soko la kisasa la Katundu juzi, lililojengwa kwa ubia baina ya Kampuni ya Geita Gold Mining Ltd (GGML) na Halmashaurti ya Mji wa Geita mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Silaa ataka mfumo mmoja kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MBUNGE wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa, ameishauri Serikali kuweka mfumo mmoja wa kielektroniki wa kuendesha shughuli zote za serikali, ambao utakuwa na taarifa za kila mtanzania.

Alitoa ushauri huo jana bungeni wakati wa mjadala wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia iliyowasilishwa na Waziri Nape Nnauye.

"Nampongeza sana Rais Samia (Suluhu Hassan) ambaye mara tatu amesisitiza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, aliyasema haya wakati akiwaapisha makatibu wakuu, alirudia tena wakati akipokea ripoti ya CAG mwaka jana na mwaka huu alisisitiza jambo hili hili," alisema Silaa.

Mbunge huyo aliipongeza serikali kwa kupiga hatua kubwa kwenye uwekezaji wa TEHAMA na kuongeza kuwa kuna kituo cha 'National Internate Data Center (NIDC), ambacho kina miundombinu mikubwa na ya kisasa katika TEHAMA.

Alisema lakini serikali kupitia Sheria namba 10 ya mwaka 2019 ilianzisha Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ambayo inafanya kazi ya kusimamia mifumo ya TEHAMA serikalini na kwamba serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha sekta hiyo inastawi. Alisema kwenye hotuba ya Waziri Nnauye kwa sasa kuna watumiaji milioni 55 wa simu na milioni 29 watumiaji wa mitandao ya 'internet' jambo ambalo ni jema, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuunganisha mifumo.

"Pamoja na hayo bado kuna shida, nchi yetu bado haina central data base system ambayo itakuwa na taarifa za kila mtanzania, tunayo NIDA anaandikisha vitambulisho, RITA anatoa vyeti vya kuzaliwa, TRA anatoa TIN Number, kuna CRB wanatoa kadi za wateja wao, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) naye aandikishe wateja hao hao," alisema.

Aliongeza kuwa hata Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unatoa kadi, polisi wanatoa leseni za udereva na kwamba kwa utaratibu huo nchi haiwezi kufika kwa urahisi inakotaka kwenda kwenye masuala ya TEHAMA kwa utaratibu uliopo.

Alisema e-government kuwa nje ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ni tatizo kubwa kwenye mfumo wa kisheria za nchi na aliishauri serikali ifanye mageuzi ili mfumo huo uwe chini ya wizara hiyo.

Mbunge huyo alisema alitembelea ofisi za e-government zilizoko chini ya Ofisi ya Rais Utumishi lakini wakati anaondoka alikabidhiwa rundo la nyaraka hali ambayo alisema ilimshangaza sana.

"Ilinishangasa sana kuona napewa nyaraka, mtu una mamlaka ya kielektroniki unaprinti nyaraka zanini? Kama kweli tuna nia ya kwenda kielektroniki tuangalie mbele zaidi, nani hapa aliwahi kuprintiwa nyaraka na facebook, nani aliwahi kuprintiwa nyaraka na instagram," alihoji Silaa.

Alisema serikali inapata hasara kubwa kwa kukosa mfumo mmoja wa kielektroniki na alitoa mfano wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwamba ina watu 155,722 ambao wanadaiwa jumla ya Sh bilioni 428 na bodi haijui itawapata wapi.

"Mheshimiwa Mwenyekiti tukisema bima ya afya kwa watu wote bila kuwa na mfumo wa kielektroniki ambao Watanzania wote watapatikana itakuwa ni ndoto hivyo lazima tuwe na mfumo wa uhakika," alisema

Kadhalika, alimpongeza Waziri Nape kwa kuleta heshima na utulivu kwenye sekta ya habari.

HABARI KITAIFA

# Mbunge ataka sheria ya habari ifumuliwe

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Ester Bulaya, jana alishikilia shilingi ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, bungeni akiwatetea waandishi wa habari kwa kutaka Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016 irekebishwe.

Hoja kubwa ya mbunge huyo ni kwamba kundi hilo kwenye baadhi ya maeneo bado linatishiwa na halifanyi kazi kwa uhuru.

Hata hivyo, Waziri Nape aliwaahidi waandishi wa habari kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 mabadiliko hayo yanakwenda kufanyika na tayari mchakato umeshaanza.

**HALI ILIVYOKUWA**

Mbunge Bulaya wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2022/23 iliyoomba kupitishiwa Sh. bilioni 282.5, alisema anataka sheria hiyo inapaswa kurekebishwa ili waandishi wa habari walikosoe taifa kwa maslahi ya kujenga nchi.

"Niseme wazi mimi ni mwandishi wa habari na nitawasemea wanahabari. Matatizo yao nayajua na nimeyaishi. Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kurudi kwake (wizarani) kaka yangu kuna nafuu, watu wamepata matumaini waandishi wenzangu.

"Na kwa kauli ya Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) imetoa matumaini kwa ile kuonyesha dhamira. Tunahitaji dhamira yako na dhamira ya Rais sasa ije kwenye vitendo kwa kuleta mabadiliko ya Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016," alisema.

"Mheshimiwa Waziri unajua mbali ya kwamba kuna unafuu lakini bado kwenye maeneo mengine waandishi wa habari wanatishwa, bado waandishi hawafanyi kazi kwa uhuru, Mheshimiwa Waziri unajua leo hakuna stori za uchunguzi kwenye magazeti wala media za kielektroniki," aliongeza.

Bulaya alisema hata makala zinazoandikwa kwa sasa ni za kawaida na kueleza kuwa sheria hiyo ikiletwa bungeni kutakuwa na mijadala ya kujenga na kukosoa Taifa.

"Tunataka turudi enzi hizo tunataka tuone makala za uchunguzi tuone vipindi mbalimbali kwenye redio na luninga, wachambuzi watakuwa huru kwa maslahi ya Taifa, haya yote hayawezi kutokea kama hakutakuwa na sheria bora ya kuwafanya waandishi wa habari wafanye kazi kwa uhuru, kufanya kazi kwa uhuru, kukiwa na uwazi Taifa letu linasonga," alisema Bulaya.

Mbunge huyo alisema lakini leo Rais Samia anaweza kumaliza muda wake na ana dhamira njema pamoja na waziri lakini wakaja wengine wasiokuwa na nia njema wakarudi kule kule kwa waandishi kuteswa, kupigwa, kunyanyaswa, kunyimwa habari kwa maslahi ya Watanzania.

"Niombe Mheshimiwa Waziri ninajua umeanza kukutana na wadau wa habari ni jambo jema lakini ninaomba zile sheria zenye ukakasi serikali mzichukie mzibadilishe kwa sababu ndiyo zinawanyima fursa waandishi wa habari.

"Kwa mfano Mheshimiwa Waziri unajua natolea tu mfano kwenye Sheria ya Huduma ya Habari kifungu cha 19,20,21 ambacho kinazungumzia kinawatambua watu gani ndiyo waandishi wa habari lakini kwenye taaluma yetu tunahitaji wanasheria, madaktari na wachumi wataandika habari kulingana na taaluma zao, lakini kwa sheria hii inataka mtu mwenye shahada ya sheria akija aanze tena kusoma habari, hapana." Alisema Bulaya na kuongeza:

"Tuna Jenerali Ulimwengu ni mwanasheria na ni mwandishi nguli, tuna (Absolum) Kibanda ni mwalimu lakini ni waandishi wazuri, tunahitaji watu wa namna hii kuja kufanya uchambuzi wa kina kwenye tasnia yetu," alisema Bulaya na kuongeza:

"Lakini watapewa miongozo inayohusu habari, kuna kifungu cha tano(e)(8)(9) kinazungumzia masuala ya leseni kinatoa mwanya wa mawaziri wenye nia mbaya kufungia vyombo vya habari, ni kifungu kibaya kuliko vyote. Tunaomba vifanyiwe kazi gazeti linatakiwa kusajiliwa tu lakini kila mwaka leseni, hiki kifungu kinatengeneza mazingira ya kufungia vyombo vya habari," alisema.

Bulaya aliongeza: "Sasa mzigo mzito kapewa Mnyamwezi wakati hii sheria mbovu inatungwa ulikuwapo na unaiona, mzigo unao mwenyewe kipindi kile kilikuwa kingine hiki ni kingine rekebisha hii sheria ili waandishi wa habari tunataka tuwe huru tulikosoe Taifa letu kwa maslahi ya kujenga ili nchi yetu iende kama nchi nyingine."




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Semina ya Wanahisa wa Benki ya CRDB, jijini Arusha jana, kuelekea Mkutano Mkuu wa 27 wa wanahisa wa benki hiyo, unaofanyika leo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika Tulia akunwa uwekezaji CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kutengeneza faida kubwa inayoiwezesha kutoa gawio kwa wanahisa wake kutokana na uwekezaji inaoufanya.

Dk. Tulia alitoa pongezi hizo wakati akifungua semina ya elimu ya fedha iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wanahisa na Watanzania kuelekea Mkutano Mkuu wa 27 wa Wanahisa utakaofanyika Mei 22, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

"Nadhani sitakuwa nimekosea nikisema ongezeko la faida baada ya kodi ambayo Benki yetu ya CRDB imepata mwaka jana kufikia Sh. bilioni 236 kulinganisha na Sh. bilioni 165 mwaka 2020, ni ukuaji mkubwa wa faida kupata kutokea," alisema Dk. Tulia.

Alisema CRDB imeendelea kudhihirisha Kwa vitendo kuwa "benki kiongozi" nchini kwa kuwa kila mwaka imekuwa ikiendelea kutoa faida ya uwekezaji kwa wanahisa wake huku akizitaka taasisi nyengine za umma na binafsi kuiga mfano.

"Nimefurahishwa pia kusikia mwaka huu Bodi ya Wakurugenzi imekuja na pendekezo la ongezeko la asilimia 64 ya gawio kwa hisa. Wanahisa wa CRDB mnastahili kutembea kifua mbele kwa ongezeko hili," aliongeza.

Dk. Tulia pia alipongeza CRDB kwa kuandaa semina ya elimu ya fedha na uwekezaji kwa ajili ya wanahisa wake na Watanzania huku akibainisha kuwa umahiri wa masuala ya fedha wa wananchi ni moja ya misingi muhimu ya maendeleo ya watu wa taifa lolote duniani.

"Niwapongeze CRDB kwa kuongoza katika utoaji wa elimu ya masuala ya fedha kwa Watanzania. Siku chache zilizopita, mliandaa semina mliyoiita CRDB Bank Uwekezaji Day. Mimi niliichungulia mtandaoni nikiwa Dodoma," alisema Dk. Tulia huku akiitaka benki hiyo kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza ujumuishi wa kifedha.

Pia aliitaka CRDB kuendelea kuwekeza katika kuendelea kuwezesha sekta mbambali za maendeleo nchini hususan sekta ya kilimo, huku akiitaka pia kusaidia malengo ya serikali katika uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ya Taifa kama ambavyo imefanya kwa Benki ya Ushirika ya Tandahimba (TACOBA) na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL).

Dk. Tulia pia aliitaka benki kuendelea na jitihada za uwezeshaji wa kundi la vijana ili kuchochea ukuaji wa ajira nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB, Dk. Ally Laay, alisema benki hiyo ikiwa ya kizalendo inayomilikiwa na Watanzania kwa zaidi ya asilimia 80, inajivunia kuendelea kukuza thamani ya uwekezaji wa wanahisa wake ikiwamo Serikali ambayo inamiliki asilimia 36 ya hisa katika benki hiyo.

"Niwakaribishe Watanzania wengine waje kuwekeza ndani ya benki yetu ili nawao waanze kunufaika na gawio nono ambalo limekuwa likitolewa na benki yao," alisema Dk. Laay.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema malengo ya semina hiyo ni kuwajengea uwezo wanahisa na Watanzania wengine ili kuwajengea uwajibikaji wa kifedha na kuongeza ushiriki katika fursa za uwekezaji hususan katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

"Kwa kutoa elimu hii wanahisa wetu pia wanapata kufahamu zaidi faida za kuwekeza katika Benki yao ya CRDB, hivyo basi kuongeza uwekezaji na kupata faida nono zaidi, lakini pia kuwahamasisha na Watanzania wengine pia kuwekeza katika hisa hususan za Benki ya CRDB na kuanza kupata gawio," alisema.

Nsekela alitumia fursa hiyo pia kuwakaribisha Wanahisa katika Mkutano Mkuu utakaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) na kupitia Mtandao. "Mkutano utaanza saa 3 asubuhi, watu wa mtandaoni wataweza kujiunga kupitia link https://escrowagm.com/crdb/login.aspx au kupitia SimBanking App," alisema Nsekela.

# Viongozi AMCOS jela kwa uhujumu

**Na Said Hamdani,** LINDI.

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi imewahukumu watumishi wawili wa Chama cha Msingi cha Ushirika Mnazi Mmoja (AMCOS), kutumikia kifungo cha miaka sita jela kila mmoja, baada ya kukutwa na hatia ya makosa mawili, likiwemo la uhujumu uchumi.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Maria Batraine, baada ya kuridhika pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Watumishi hao ni, Sofia Hamisi Nambea ambaye ni karani wa chama hicho na Mjumbe wa Bodi wa AMCOS, Ally Abdi Ally.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Batraine aliwapa washitakiwa nafasi ya kujitetea kila mmoja, wote waliomba waonewe huruma kwa madai ni wakosaji wa mara ya kwanza pia wana familia zinawategemea.

Baada ya utetezi huo Halimu Batraine alimuuliza Mwendesha Mashitaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Osborn Pois iwapo wana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washitakiwa hao.

Hata hivyo, Pois alimweleza hakimu kwamba hana, huku akiiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa hao ili iwe fundisho kwa upande wao na wengine waliokuwa na tabia ya aina hiyo

"Hakimu sina kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washitakiwa, lakini naiomba mahakama yako tukufu iwape adhabu kali washitakiwa hawa ili iwe fundisho kwao ikizingatiwa tabia ya wizi inaendelea kushamiri," alisema Pois.

Hakimu Batraine akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 02/2021, kosa la kwanza likiwa ni wizi amewahukumu kupitia kifungu cha 258 (1) cha sheria kulipa faini ya Sh.500,000 na wakishindwa watumikie kifungo cha miezi (12) kila mmoja. Kosa la pili ni kuisababishia AMCOS hasara kupitia kifungu cha 57 (1) na 60 kifungu kidogo (2) vya sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019, aliwahukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitano pamoja na kulipa faini ya Sh. milioni 7.6 kila mmoja.

Pia Hakimu Batraine aliwaeleza washitakiwa hao nafasi ya kukata rufaa ipo wazi iwapo hawajaridhishwa na hukumu waliyopewa na mahakama hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Sekta binafsi, TAMISEMI vinara rushwa

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni imetaja taasisi zinazoongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa, kinara ikiwa ni sekta binafsi ikifuatiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Maeneo mengine yaliyolalamikiwa ni Mahakama, Polisi, Ardhi na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Elizabeth Mokiwa wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yao kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Mokiwa alisema katika kipindi hicho kesi 162 zilipokelewa wakilalamikia vitendo vya rushwa katika taasisi hizo.

Mokiwa alisema katika kesi hizo malalamiko kwa sekta binafsi yaliyopokelewa yalikuwa 68, TAMISEMI 24, Ardhi 15, Polisi 13, Mahakama 13, TBS 11 na malalamiko 16 yalihusu mtu mmoja mmoja.

Aidha, alisema katika kipindi hicho wamefuatilia miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 11 kwa lengo la kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika kwa usahihi kwa kuzingatia ubora, thamani ya fedha na muda uliopangwa.

Hivyo, Mokiwa aliwataka wananchi wa Kinondoni na Ubungo kutumia vizuri siku za kusikiliza malalamiko na kero zilizotengwa na taasisi hiyo, lengo likiwa ni kuhakikisha vitendo vya rushwa vinatokomezwa.

Aidha, Mokiwa alisema kufanikisha mikakati yake TAKUKURU imejipanga kushirikiana na Chama cha Skauti chini ya Mpango wa TAKUSKA kwa kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwamo umuhimu wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

# TAMWA yalaani kushamiri matukio ukatili kwa watoto

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), kimelaani matukio ya ukatili wanayoendelea kufanyiwa watoto katika maeneo mbalimbali nchini na kuitaka serikali kufanya mabadiliko ya sera na sheria za kuwalinda.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, aliyaeleza hayo jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari na kusema kuwa kunzia Januari hadi Mei mwaka huu matukio matano yaliripotiwa.

Alitaja aina ya matukio hayo kuwa ni lililotokea mkoani Katavi la mwalimu wa mafundisho ya dini ya kikristo, Joseph John kuwalawiti watoto wanne.

Alisema lingine ni mkazi wa Iringa aliyedaiwa kumlawiti mtoto wake wa kambo, watoto 14 kulawiti watoto wenzao 14 wa kiume na tukio la mwalimu wa madrasa Jumanne Ikungi, mkazi wa Arusha kuwalawiti wanafunzi 22 wa Shule ya Msingi Mkonoo.

"Kwa matukio haya yaliyoripotiwa kati ya Januari hadi Mei, inatosha kusema kuwa watoto wetu hawapo salama na TAMWA tunalazimika kusema, watoto hawa hawana pa kukimbilia.

"Mwenendo huu wa matukio ya ubakaji na ulawiti wa watoto tena na walimu, viongozi wa dini, wazazi na walezi, unadhihirisha kuwa tatizo hili bado ni kubwa nchini na linahitaji uamuzi mgumu kutoka kwa watunga sera wetu," alisema Dk. Reuben.

Alisema kuwa, pamoja na wadau wengine wa masuala ya jinsia wamekuwa wakiimba na kuitaka jamii kuzuia ukatili kwa miaka zaidi ya 30 hasa wakililia mabadiliko ya sera, sheria na kutoa elimu kwa jamii.

Aidha, alisema taarifa za makosa ya ukatili wa jinsia na unyanyasaji zilizotolewa na Jeshi la Polisi katika chama hicho mwaka jana, zilionyesha mikoa ya kipolisi iliyoongoza kwa ukatili dhidi ya watoto ni Arusha 808, Tanga 691, Shinyanga 505, Mwanza 500 na Ilala 489.

Aliongeza kuwa, makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ya matukio ni ya ubakaji 5,899, kumpa mimba mwanafunzi 1,677, ulawiti 1,114, kumzorotesha mwanafunzi masomo 790 na shambulio 350.

Alisema utafiti uliotolewa hivi karibuni na taasisi ya Haki Elimu, unaonyesha kuwa watoto wengi hawafundishwi elimu ya afya ya uzazi, lakini zaidi sasa walimu nao wanaogopa kufundisha wanafunzi mada hizo.

# Bashungwa awaagiza makatibu kujadili matatizo ya machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amewaagiza makatibu wakuu wa wizara za kisekta kukutana na kujadili fursa na matatizo yanayowakabili machinga nchini ili serikali izifanyie kazi.

Bashungwa alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha Jukwaa la Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2022.

Kikao hicho pia kilitumika kujadili na kuweka mikakati ya serikali kuliwezesha kundi la machinga nchini.

Alisema serikali imejikita katika kuliwezesha kundi la machinga kwa kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara.

Bashungwa alisema baada ya kikao hicho kuisha makatibu wakuu wa wizara za kisekta wanatakiwa kukutana haraka ili kujadili matatizo na fursa zilizopo kwa machinga.

"Baada ya kikao hiki natoa maagizo kwa makatibu wakuu wa wizara za kisekta sisi TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya jamii, kukutana haraka ili kujadili matatizo na fursa ili serikali iweze kuzifanyia kazi.

"Lakini pia mtafute mapendekezo na kuja na majibu yatakayo jibu kero za kundi hili pia kuona ni vitu gani ambavyo vinaweza kukwamisha mikakati na jitihada za serikali inayofanywa na serikali,"alisema Bashungwa

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika mazungumzo na Serikali ya India ili kupata mkopo wa masharti nafuu utakaotumika kuwezesha machinga. Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Mwanaidi Ally Hamisi, alimshukuru Rais Samia kwa namna ambavyo anaendelea kuliinua kiuchumi kundi hilo.

Vilevile, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali bado zipo kero za mazingira yasiyo rafiki, mitaji, bajeti, ujuzi stahiki wa kufanya biashara kwa machinga, stadi za kazi na huduma rafiki.

Kadhalika alizitaka taasisi za fedha nchini kuweka viwango vya chini vya riba za mikopo ili kuwezesha machinga kupata mikopo na kukuza mitaji yao.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UTAMADUNI WA USALAMA MAHALA PA KAZI KWA EACOP LTD KWA TANZANIA**
**KUMBUKUMBU NO: 10007720**

Kampuni ya EACOP Ltd inahitaji huduma kutoka kwa wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika kuwezesha utayarishaji wa mpango wa utamaduni wa usalama mahala pa kazi kwa kampuni na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 296 ziko Uganda na 1,147 ziko Tanzania.

Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Tanzania itahusisha vituo 4 vya pampu, vituo 2 vya kupunguzia kasi ya mtiririko wa mafuta; kituo kikuu cha kuhifadhia mafuta karibu na bahari (Marine Storage Tank) na kituo cha kupakilia mafuta (Load Out Facility); kambi 12 za wafanyakazi na za kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi; na vituo vya kuvunia mwanga wa jua (solar farms). Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Uganda itahusisha vituo 2 vya pampu; kambi 4 za wafanyakazi na za kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi.

EACOP Ltd ilianzishwa tarehe 15 Februari 2022 na hatimaye itahusisha hadi watu 6,000 kutoka kwa wakandarasi na wakandarasi wasaidizi kutoka katika mataifa na tamaduni mbalimbali, yaliyosambaa kutoka sehemu mbalimbali za kijiogorafia.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Dhamira ya kampuni ni kuhakikisha usalama mahala pa kazi wa watu na mali, kuhifadhi maliasili na kulinda mazingira halisi na ya kibinadamu kwa kushirikiana na wenyeji huku ukidumisha utiifu wa kanuni zote zinazotumika na vibali vinavyotolewa na wadhibiti. Lengo la kampuni ni kutokuwa na madhara kwa watu, mazingira, kwenye jamii inapofanyia kazi, na mali zake na kwa sifa ya kampuni. Kampuni kwa sasa inaanzisha mifumo yake ya usimamizi, michakato na ingependa kuunda utamaduni wa kiwango cha kimataifa wa afya, usalama mahala pa kazi na mazingira (HSE).

EACOP inahitaji huduma za makampuni au mashirika yenye uzoefu na yenye sifa nzuri ili kusaidia EACOP Ltd kuandaa mpango bora wa utamaduni wa usalama mahala pa kazi kwa kampuni na mradi wa EACOP Ltd. Lengo litakuwa kwa EACOP na wakandarasi wao kuendeleza utamaduni dhabiti wa usalama katika mradi wote kwa kutumia lugha moja na zana kwa pamoja na wakandarasi.

Vigezo muhimu ambavyo vitazingatiwa katika uchaguzi wa program ya utamaduni wa usalama inayopendelewa itajumuishwa:

- Progamu inayowezesha tamaduni dhabiti ya usalama mahala pa kazi ambayo itaongeza ushiriki wa wafanyakazi, na utashughulikia usalama mahala pa kazi, mazingira, jamii, ubora na ufanisi wa kazi.
- Programu ambayo inajenga mawazo ya 'kufahamu hatari' ili kuwaweka wafanyakazi na familia zao salama kazini, nyumbani na barabarani.
- Programu ambayo inafaa kwa wafanyakazi wengi na wa tamaduni mbalimbali ambao wana uelewa mdogo sana wa hatari na utamaduni mdogo wa usalama mahala pa kazi.
- Programu ambayo ni rahisi, inayonyumbulika na ya haraka kutekelezwa (ndani ya miezi si miaka)
- Programu inayofaa kwa miradi mikubwa na/au mashirika yanayo anza kufanya kazi.
- Programu inayoweza kufasiliwa kwa ajili ya EACOP na hatari pamoja na changamoto za miradi.
- Programu yenye rekodi bora na utekelezaji wa HSE (miradi mikubwa ya kimataifa).
- Uzoefu na uwezo wa washauri maalumu/wakufunzi walio pendekezwa kwa EACOP.

216865001

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yatakayo onyesha nia yanatakiwa kuwa na vielelezo vifuatavyo:

- Uzoefu/utendaji katika kutoa programu sawa za utamaduni wa usalama zilizoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania/Uganda, au kwa angalau uzoefu na utendaji bora wa miaka 10 kwa huduma inayofanana na hiyo kimataifa
- Wafanyakazi waliofuzu na wenye uzoefu wa kutekeleza program za utamaduni wa HSE kwa miradi mikubwa ya gesi na mafuta.
- Uzoefu wa kutengeneza programu za kitamaduni za HSE ambazo hutoa utendakazi wa kiwango cha kimataifa cha HSE
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa akaunti za fedha za muda wa miaka mitatu iliyopita
- Muonesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia yake ni muhimu sana
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, Usalama mahala pa kazi na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani ya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa leseni unaofaa kutoka kwa mamalka husika ndani ya nchi kwa ajili ya huduma
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania na cheti kinachoonyesha uthibitisho ulipaji wa kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.

Makampuni yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** saa au kabla ya saa **10 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **31 Mei 2022.** Ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb.** Taarifa zote ziwasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho. Taasisi zitakazokidhi vigezo ndizo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serengeti Girls mpeni heshima Mama Samia

**KIKOSI** cha Timu ya Soka ya Taifa ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kiliondoka nchini jana kuelekea Cameroon kuwakabili wenyeji katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), itakayochezwa kesho.

Timu hizo zitarudiana wikendi ijayo na mshindi wa jumla atafuzu kucheza fainali za Kombe la Dunia za U-17 zitakazofanyika baadaye mwaka huu huko India.

Serengeti Girls ni moja kati ya timu sita zilizofika hatua ya mwisho ya kusaka wawakilishi watatu kutoka Afrika watakaofuzu fainali hizo, timu nyingine zilizofika hatua hiyo ni Ethiopia ambayo yenyewe itacheza dhidi ya Nigeria wakati Ghana watapambana na Waarabu wa Morocco.

Hadi kufikia hatua hii, inaonyesha Serengeti Girls wamepambana vyema kusaka tiketi hiyo, hivyo wanastahili kuungwa mkono ili kufikia malengo na ndoto za Watanzania ambazo zimedumu kwa muda mrefu.

Licha ya kutokuwa na wadhamini, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limepambana kuhakikisha Serengeti Girls inafanya mazoezi kwa mujibu wa programu zake zilizoandaliwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, wachezaji wanapata vifaa na chakula kwa wakati.

Ingawa timu hiyo ilisafiri jana, lakini bado inahitaji kupata huduma muhimu ili wachezaji wake waishi maisha yanayofanana na kazi ya kulitumikia taifa wanayoifanya.

Tunapenda kuwakumbusha wadau kujitokeza sasa kuwasaidia Serengeti Girls ili kurahisisha maandalizi yao na hatimaye kupata nafasi ambayo wanaililia kwa muda mrefu ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza.

Wachezaji wanapopata maandalizi sahihi sasa, yatasaidia kufuzu lakini pia yatawafanya waende katika fainali hizo (endapo wataifunga Cameroon), wakiwa imara kila idara na si kusindikiza mataifa mengine.

Kesho watakuwa na dakika 90 za ugenini, halafu watarejea nyumbani kumalizia dakika kama hizo zilizobakia. Ni mechi ngumu lakini katika mchezo wa soka hakuna kisichowezekana.

Nipashe inawaomba wadau wa michezo nchini na Watanzania wote kuiombea dua njema timu hii ili itimize ndoto zake lakini pia impe heshima Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan.

Kufanya vizuri kwa timu hiyo kutaweka rekodi nyingine kwa nchi kwa sababu ikiwa chini ya Rais ambaye ni mwanamke, itakuwa pia imefuzu tiketi ya kushiriki fainali hizo zinazohusika soka la wanawake duniani.

Ushirikiano na umoja wa kweli unahitajika zaidi wakati huu ambapo Tanzania na TFF iliyoko chini ya Rais, Wallace Karia imepiga hatua, hivyo kama kuna tofauti zozote au mgawanyiko, usipewe nafasi kipindi hiki ambacho Serengeti Girls imekaribia kukata tiketi hiyo adimu na inayosubiriwa kwa muda mrefu.

Wote tunafahamu mpira wa miguu wa wanawake umebadilika na huu ni muda sahihi kwa makampuni na taasisi zenye uwezo kuisaidia timu hii ili ifanye vyema majukumu yake na hatimaye kutulika kiu cha Watanzania ambao hawajawahi kuona Tanzania inashiriki fainali zozote za dunia.

Tunaamini benchi la ufundi limefanya kazi yake vyema na wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza mechi ya kesho na ile ya marudiano watajituma na hatimaye kuvuna matokeo chanya.

Nipashe inawakumbusha wachezaji wa Serengeti Girls kufahamu hatua ambayo wamefikia ni kubwa lakini wanatakiwa kuendelea kujituma kwa sababu kwa kufanya hivyo wanaweza kujifungulia milango kwa kuwavutia mawakala kuwasajili na hapo ikawa mwanzo wa kubadilisha maisha yao ya kisoka.

**Mungu ibariki Serengeti Girls, Mungu ibariki Tanzania.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kufungiana miaka 5 si sawa

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara nyingine tena tumeona watu wa familia ya soka wakifungiwa miaka mitano kujihusisha na masuala ya mpira wa miguu.

Mara ya mwisho ilikuwa ni mwanzoni mwa Aprili, 2021 wakati Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela alipofungiwa miaka mitano, lakini alifunguliwa baadaye baada ya kukata rufaa na malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa soka nchini.

Tumeona wiki hii, Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Mbwana Makata na meneja wake, David Naftali wakifungiwa kujihusha na masuala ya soka kwa kipindi cha miaka mitano.

Adhabu hiyo ilitolewa na Kamati ya Utendaji na Usimamizi wa Ligi, ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), baada ya kuwakuta na hatua ya kushawishi/kuamuru wachezaji wasiingie uwanjani kuanza mchezo huo, tukio lililosababisha mchezo wa timu yao dhidi ya Namungo FC kutofanyika.

Mechi hiyo ilikuwa ifanyike kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi Mei 13,mwaka huu lakini haikuchezwa kwa sababu hizo.

Kamati ikadai baada ya kupokea taarifa na ilifanya uchunguzi na kubaini gari hilo lenye namba STL 3096 lilifika uwanjani hapo, lakini liliondoka kwa dharura kabla ya muda wa mchezo kuanza.

Ikasema waandaaji wa mchezo, Chama Cha Soka Mkoa wa Lindi (LIREFA), kwa kushirikiana na kamisaa walikubaliana kutafuta gari linaloweza kutumia kubeba majeruhi kabla gari hilo maalum halijarejea, lakini walipinga, pamoja na gari hilo kurejea kabla ya muda.

"Cha msingi nimeiona taarifa hiyo kwenye vyombo vya habari, nadhani kuna utaratibu wa kupata barua rasmi na mambo mengine yatafuata. Adhabu nimeiona, nitajua la kufanya baada ya kukaa na kutafakari pale nitakapopata barua, kuangalia vifungu ambavyo vimetumika kunifungia, ndiyo nitajua sasa nifanye nini, kwa sasa siwezi kufanya au kuongea chochote, ila baadaye nikakapopata hiyo barua na kuona inaeleza nini, nikiona sijatendewa haki kitakata rufaa, kama nikiona ni sahihi kilichofanyika, basi nitajua la kufanya," alisema Makata siku moja tu baada ya kamati kutoa taarifa hiyo.

Naunga mkono adhabu kwa Makata kwa sababu alichokifanya hakikubaliki kwenye dunia ya sasa ya soka.

Soka kwa sasa ni biashara kubwa, watu wamelipa matangazo kwa ajili ya kuonyesha kwenye televisheni, kuna waliolipia ving'amuzi kwa ajili ya kuonyesha mpira, lakini kuna wale ambao wameshalipa viingilio kwenye mabaa, na vibanda umiza. Wote hawa wamepata hasara baada ya mechi hiyo kutoonyeshwa. Kila mtu analia kivyake. Haya yote wamesababisha na mtu mmoja au wawili kwa sababu zake za kutaka mechi isichezwe. Hapa adhabu ni lazima.

Hata hivyo, adhabu hiyo naiona ni kubwa mno. Adhabu kama hizo hutolewa kwa wapanga matokeo na si vinginevyo.

Makata na mwenzake ni kweli wanastahili adhabu, lakini siyo ya kumfungia miaka mitano.

Nadhani bado Watanzania tunaendelea kuishi kwenye dhana za ujamaa, ambazo kwa sasa kwenye nchi yetu kwenye sehemu nyingi hazifanyi kazi.

Zamani soka lilikuwa ni burudani, kujenga afya, mwili, kudumisha upendi na umoja na si kama kama hivi sasa.

Ndiyo maana wachezaji. makocha walikuwa wako Simba, Yanga au Pan African, lakini walikuwa wanafanya kazi kwenye taasisi na mashirika mbalimbali na umma.

Wanacheza au kufundisha huku wakifanya kazi. Kwa hiyo hata akifungiwa miaka mitano au kumi, anaendelea na maisha yake kama kawaida. Ni adhabu ambazo zilikuwa hazimuathiri kwenye maisha yake kama binadamu. Ndiyo maana wakati huo wachezaji walikuwa wakifungiwa miezi mitatu, sita au mwaka, lakini kwa sasa huwezi kuiona hilo hata hapa nchini, achilia mbali CAF na FIFA.

Lakini kwa dunia ya sasa soka ni ajira, ambayo mtu anaishi na kuendesha familia yake, ukimfungia kwa miaka hivyo si kutomtendea haki, ila unakiuka haki zake kama biandamu.

Mtu mwenye mke, watoto na familia, unapomfungia asifanye kazi anayeoiweza, ni kama kumfunga mikono tu.

Mimi nilidhani kamati hiyo iangalie upya, hizo ni adhabu za kizamani sana, wakati huo soka haikuwa kazi rasmi.

Pia nashangazwa na kanuni hiyo kuwepo hadi leo. Nilitegemea wadau wa soka wanaoitwa ili kuzirekebisha kila msimu wangeipigia kelele iondolewe, lakini kumbe bado ipo.

Labda viongozi wa Simba na Yanga wao wanaona kanunu hiyo haiwezi kuwabana, lakini wa mikoani nao vipi? Wanaendelea kuiachia tu kanuni hii iliyopitwa na wakati na kuikumbuka pale inapowakuta?

Wanapofanya marekebisho kanuni za kila mwaka nini wanachokifanya? Au wanachokumbuka ni kuitetea tu kanuni ya kuchukua pesa zote za mapato kwenye mechi ambazo Simba na Yanga zinacheza mikoani?.

HABARI BUNGENI

# Hoja saba Muungano bado ufumbuzi

BUNGE limeelezwa kuwa hoja saba za Muungano bado hazijapatiwa ufumbuzi hadi sasa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Fuoni (CCM), Abbas Hassan.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji hoja gani za Muungano ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi mpaka sasa na ni jitihada gani za makusudi zinafanyika ili kero zilizosalia zipate ufumbuzi.

Akijibu swali hilo, Dk. Jafo alitaja hoja hizo kuwa ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu na usajili wa vyombo vya moto.

Zingine, alisema ni ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, kodi ya mapato (PAYE) na kodi ya zuio (withholding tax), mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha na hoja ya uingizaji wa sukari katika soko la Tanzania Bara.

Hata hivyo, alisema zipo jitihada za makusudi zinazofanyika ili hoja zilizosalia zipate ufumbuzi.

Alibainisha jitihada hizo ni kwamba ofisi imeendelea kuimarisha uratibu wa utatuzi wa hoja zilizobaki kati ya sekta zenye hoja za pande zote mbili za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na SMZ na kuwasilisha uamuzi kwenye sekretarieti ya kamati ya pamoja yenye jukumu la kufuatilia hatua za utekelezaji wa maagizo ya kamati ya pamoja na kutoa ushauri kwa sekta zenye hoja namna ya kuendelea kutatua hoja hizo.

Pia alisema serikali za pande zote mbili zinashirikiana kwa karibu kuhakikisha vikao vya pamoja vilivyokubaliwa kwa ajili ya kutafutia ufumbuzi hoja zilizosalia vinaendelea kama utaratibu ulivyopangwa.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga, alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kutumia neno changamoto badala ya kero kwenye suala hilo la Muungano.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alikubali ushauri wa mbunge huyo na kudai kuwa kwa sasa neno linalotumika ni hoja za Muungano na si kero



## Mbunge alia na umeme vijijini

MBUNGE wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga ametaka serikali kupeleka umeme kwenye vijiji 31 vya jimbo hilo ambavyo hadi sasa havijafikiwa na huduma hiyo.



Akiuliza swali bungeni jana, Hasunga alisema vijiji hivyo bado havina umeme na Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo takribani mwaka mmoja umepita hajafikisha umeme kwenye maeneo hayo.

"Je, serikali inatuhakikishiaje kufikia Mwezi Desemba mwaka huu vijiji hivyo vitakuwa vimefikiwa na umeme?" alihoji.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema mradi wa upelekaji umeme vijijini chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uko kwenye awamu tofauti.

"Kuna awamu ya kumpata mkandarasi tunaposaini (tunapotia saini) mkataba, kwenda kukagua maeneo na kuona uhalisia wake lakini tunarudi mezani mkandarasi, TANESCO na REA wanakubaliana namna ya kazi ifanyike halafu hatua ya tatu ni kuagiza vifaa na hatua ya nne ni kuanza kufanya kazi," alisema. Byabato alisema anaamini kwenye jimbo hilo kuna hatua zinaendelea na matarajio ifikapo Desemba, mwaka huu, umeme uwe umefika kwenye maeneo hayo.

Byabato alisema serikali itahakikisha inakabana na wakandarasi ili kufikisha umeme kwenye maeneo yote kwa kuwa vifaa vimeshanunuliwa, hivyo kazi zilizopangwa zitakamilika.




Habari zote na Augusta Njoji



Mbunge wa jimbo la Ukonga, Jerry Silaa, akiuliza swali la nyongeza kwenye kipindi cha maswali na majibu katika Bunge la bajeti linaloendelea, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Tathmini yafanywa miundombinu shule kongwe

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza kufanya tathmini ya hali ya miundombinu ya shule zote za msingi zikiwamo kongwe zilizoanzishwa kabla ya Uhuru mwaka 1961. Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mwandabila.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kukarabati shule za msingi za zamani ambazo majengo yake yamechakaa na kuharibika wilayani Ileje na Mbozi mkoani Songwe.



Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema tathmini hiyo inafanyika kupitia mradi wa BOOST ili kubaini mahitaji ya ujenzi wa miundombinu mipya ya shule na hali ya uchakavu wa miundombinu iliyopo.

"Tathmini hiyo imeanza Aprili, 2022 na itakamilika Julai, 2022. Matokeo ya tathmini hiyo yatatumika kuandaa mpango wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi mwaka 2025/26,"alisema.

Awali, alisema kuna shule 2,147 za msingi kongwe nchini ambazo zilianzishwa kabla ya Uhuru mwaka 1961, hali ya miundombinu ya shule hizo ni mseto zikiwamo zenye hali nzuri na zingine zenye miundombinu chakavu.

Kuhusu shule kukosa vyoo, Silinde alisema katika mwaka ujao wa fedha, serikali hiyo imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, alisema katika jimbo lake kuna shule nyingi sana za msingi ambazo ni kongwe na zimekuwa zikifanywa juhudi na wananchi kukarabati. "Naomba kumuuliza Waziri lini huo mpango wa kukarabati hizi shule kongwe utaanza?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema mara baada ya kukamilika kazi ya tathmini utekelezaji wake utaanza na watafikia shule zote.

# NIMR yazindua maabara ya kisasa vinasaba malaria

Na Mary Geofrey

TAASISI ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupitia Mpango wa Taifa wa Magonjwa ya Kudhibiti Malaria, imezindua maabara ya kisasa, kwa ajili ya kuzalisha takwimu za vinasaba na kuzichakata.

Aidha, wanafanya utafiti wa kufuatilia Malaria kwa kutambua mbinu za vinasaba.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, aliyaeleza hayo jana wakati akizindua maabara hayo jana jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Alisema maabara hiyo pia itaongeza msukumo kwenye ufuatiliaji wa Malaria ili kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

"Pamoja na mafunzo kwa wataalamu, ufadhili huu umejenga maabara hapa NIMR kwa ajili ya kuzalisha takwimu za vinasaba na kuzichakata," alisema Sichwale huku akibainisha kuwa wanategemea kutumia maabara hiyo katika kuzuia na kufuatilia magonjwa mengine.

Alisema utafiti huo unafadhiliwa na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation kuanzia Mei mwaka 2020 na utakamilika Oktoba 2023.

Dk. Sichwale alisema utafiti huo unafanywa kwenye mikoa 13 ya Tanzania Bara, ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Mara, Manyara, Mtwara, Njombe, Songwe, Ruvuma, Tanga na Tabora.

Alisema wanazungumza na wafadhili kuendelea kufadhili mradi huo hata pale muda wa mradi utakapomalizika mwakani.

Vile vile, alisema wanawakaribisha wadau wengine kufanya kazi na serikali ili kufanya utafiti wa Malaria utakaoleta matokeo chanya.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Paul Kazyoba, alishukuru serikali na wadau walioshiriki katika ujenzi huo wa maabara na kufanya utafiti wa vinasaba vya ugonjwa huo.

Alisema maabara hiyo itawawezesha kupata takwimu za kina kuhusu ugonjwa huo na kuahidi kusimamia utekelezaji wake.

Kazyoba alisema maabara hiyo kubwa itakayotumika kupima sampuli mbalimbali ina mashine za kisasa za kufanya uchunguzi wa vinasaba.

"Tunaamini maabara hii itaisaidia serikali kupata matokeo chanya ya tafiti zake kwa maslahi mapana ya Taifa," alisema Kazyoba.



Mmoja wa viongozi wa dini walioshiriki katika uzinduzi rasmi wa msimu wa uzalishaji sukari 2022/23 katika kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSCL), mkoani Morogoro mapema wiki hii, akitoa sala fupi kubariki shughuli za uchomaji mashamba na uvunaji wa miwa. Wengine ni kikosi maalumu cha uchomaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilombero yazindua msimu wa uzalishaji

Na Mary Geofrey

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha sukari inapatikana kwa wingi nchini, Kampuni ya Sukari ya Kilombero, imezindua msimu wa uzalishaji kwa mwaka 2022/23, ikiwa ni wiki moja mapema zaidi ya matarajio ya awali.

Msimu mpya wa uzalishaji unaanza mapema kufuatia kukamilika kwa hatua za matengenezo ya kiwanda na matarajio ya awali yalikuwa kukamilisha matengenezo katika wiki ya mwisho ya mwezi Mei.

Akizungumza katika hafla fupi ya uzinduzi wa msimu wa uzalishaji, Mkuu wa Idara ya Uhusiano, Ephraim Mafuru alisema; "Timu zetu zimefanya kazi kubwa ili kuhakikisha kuwa matengenezo ya kiwanda yanakamilika ndani ya muda uliopangwa. Tuna furaha kutangaza kuwa tuko tayari na tunaanza uzalishaji wa sukari ikiwa ni mapema zaidi ya matarajio ya awali."

Maofisa mbalimbali wa kampuni, viongozi wa kidini na baadhi ya wananchi walihudhuria tukio rasmi la kuzindua msimu wa uzalishaji ambalo hujulikana kama 'first burn'.

"Kama kampuni tuna mikakati mbalimbali ya kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii muhimu. Kuanza uzalishaji mapema ni hatua kubwa na kwa sasa iko katika mradi wa upanuzi ambao unatarajiwa kukamilika Juni 2024 na utaongeza uwezo wa kampuni kuzalisha sukari mara mbili zaidi na kupunguza uhaba wa sukari nchini kupitia chapa ya Bwana Sukari."

# Adha ya maji Mabwepande kuwa historia

Na Joseph Mwendapole

WAKAZI wa Mtaa wa Mbopo, Kata ya Mabwepande mkoani Dar es Salaam, wanatarajia wataondokana na shida ya maji baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) kuanzisha mradi wa kuwafikishia huduma ya majisafi kwa mara ya kwanza

Hatua hiyo inatokana na utekelezaji wa mradi wa maji Makongo hadi Bagamoyo unaoendelea kutekelezwa na DAWASA chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Msimamzi wa mradi huo, Mhandisi Juma Kalemera, alisema hayo juzi wakati akielezea utekelezaji wa mradi huo kwa eneo la Mbopo linalotarajiwa kuanza kupata huduma ya majisafi ifikapo Juni 2022.

Alisema kazi inayoendelea kwa sasa inatoa matumaini kwa wananchi wa Mbopo kupata huduma ndani ya muda uliopangwa.

"Kwa sasa mkandarasi anayetekeleza mradi huu CDEIC & HAINAN JOINT VENTURE anaendelea na kazi ya kufunga mita za maji kwa wateja ili tutakapo ruhusu maji kwenda kwa wananchi yawafikie miundombinu ikiwa imekamilika ili waweze kupata huduma kwa wakati," alisema Kalemera.

Mhandisi Kalemera aliongeza kuwa hadi sasa zaidi ya mita 300 za maji zimefungwa huku zaidi ya wananchi 3,000 wakitarajia kunufaika na huduma ya majisafi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbopo, Mohammed Bushiri alishukuru Serikali kupitia DAWASA kwa kutekeleza mradi mkubwa utakaoleta nafuu ya maisha kwa wananchi ambao awali walikuwa wanatumia maji kutoka kwa watu binafsi.

"Utekelezaji wa mradi huu unaonesha ni jinsi gani Serikali yetu ilivyo sikivu na kuwajali wananchi wake, leo Mbopo tuna matumaini makubwa hivi karibuni tunaenda kupata huduma ya majisafi, lakini zaidi mradi huu hautunufaishi wakazi wa Mbopo tu bali kuna maeneo mengine mengi ambayo hayakuwa na huduma," alisema Bushiri.

Rashid Kawa, Mkazi wa Mbopo alisema kwa muda mrefu wamekua hawana huduma ya majisafi huku wakitumia gharama kubwa kupata maji kwa watoa huduma binafsi.

"Tumeishi kwa muda sasa bila huduma ya majisafi huku Mbopo, gharama za maisha zimekua juu kwa kuwa maji tumekua tukinunua kwa bei ghali toka kwa watoa huduma binafsi, tutakapoanza kupata maji sasa maisha yataimarika sana," alisema

Mradi wa maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo unatekelezwa kwa gharama ya shilingi Bilioni 65.4 na unatarajiwa kuhudumia wakazi wapatao 450,000 katika maeneo ya Changanyikeni, Vikawe, Goba, Bunju, Wazo, Ocean Bay, Salasala na Mji wa Bagamoyo.



HABARI DODOMA

# Watalii waongezeka zaidi kuanzia Januari hadi Aprili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema idadi ya watalii waliongia nchini kutoka nchi za nje kwa kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu imeongezeka.

Kaimu Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa takwimu za watalii kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka.

Alisema idadi ya watalii walioingia nchini kuanzia Januari hadi Aprili, mwaka huu, ni 367,632 ambao walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii ikilinganishwa na watalii 275,097 walioingia nchini mwaka 2021.

Kwa mujibu wa masolwa, hilo ni ongezeko la watalii 92,535 sawa na asilimia 33.6 kati ya watalii 367,632 walioingia nchini ni watalii 124,212 waliingia nchini kupitia Zanzibar ambapo ni sawa na asilimia 33.8 ya watalii wote.

Masolwa alisema kuwa watalii walioingia Aprili mwaka 2022 waliongezeka hadi 78,784 kutoka watalii 43,966 walioingia nchini mwaka jana kipindi kama hicho.

"Idadi ya watalii waliooongezeka walikuwa 34,818 sawa na asilimia 79.2, ongezeko hilo limetokana na nchi nyingi duniani kuondoa zuio la kusafiri kutokana na kupungua kwa hali ya maambukizi ya UVIKO -19 na juhudi za serikali kuendelea kutangaza vivutio vya utalii nchini," alisema Masolwa

Akizungumzia watalii walioingia nchini kabla na baada ya UVIKO-19, alisema walioingia nchini mwaka 2019 walikuwa 1,510,151 ambapo idadi kubwa zaidi ya watalii 160,296 waliingia nchini Desemba 2019.

"Baada ya dunia kukumbwa na UVIKO-19, nchi nyingi ziliweka vikwazo vya kusafiri vilivyosababisha idadi ya watalii walioingia nchini kupungua hadi 620,867 mwaka 2020 ambayo ni idadi ndogo zaidi ya watalii 7,105 waliingia nchini mwezi Aprili 2020.

"Mwaka 2021 idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka hadi 922,692 sawa na asilimia 48.6 aidha idadi ya watalii wanaotarajiwa kuingia nchini itaongezeka zaidi ya idadi ya iliyokuwapo kabla ya UVIKO-19 kutokana na juhudi za serikali kutangaza vivutio vya utalii ambavyo ni pamoja na mbuga za wanyama,fukwe za bahari, mlima Kilimanjaro, uwindaji na utalii wa kitamaduni," alisema Masolwa.



Ofisa Mkuu Mawasiliano na Mahusiano wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mabel Masasi (kulia), akitoa maelezo ya shughuli za mamlaka kwa mteja aliyetembelea maonyesho ya Wiki ya Maadhimisho ya Ubunifu, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavumbuzi watakiwa kusajili kazi kwa ulinzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Miliki Bunifu ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Seka Kasera, amewataka wavumbuzi kujijengea utaratibu wa kulinda kazi wanazobuni kisheria kwa kuzisajili ili ziwe salama.

Kasera alisema hayo katika maonyesho ya Wiki ya Ubunifu, yanayoendelea katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kwa kushirikisha wabunifu kutoka mikoa mbalimbali nchini. Alisema ili wavumbuzi wawe na uhakika na usalama wa kazi za ubunifu wanazofanya wanapaswa kufuata taratibu za kuzisajili katika mamlaka husika.

"Ulinzi kwa kitu unachokifanya ni muhimu sana hivyo ni vema wavumbuzi kuhakikisha wanasajili na kuweka ulinzi wa bunifu zao kisheria kwa kusajili kwa wakala," alisema Kasera.

Alifafanua kuwa baada ya kutembelea katika mabanda ya maonyesho yaliyopo katika uwanja huo wamebaini kuwapo kwa bunifu nyingi zenye sifa ya kupata ulinzi ambazo zimebuniwa na vijana wadogo.

"Tumeweza kupitia baadhi ya mabanda kuangalia bunifu na ambazo zimepata ulinzi kutokana na kuwa tumezisajili lakini kuna ubunifu mwingine una sifa ya kupata ulinzi na mwingi ni wa vijana wadogo, ubunifu huu ukipata ulinzi utaweza kupata soko la kitaifa na kimataifa," alisema Kasera.

Kutokana na hilo alisema katika maonyesho hayo wanatoa ushauri hivyo wabunifu wajitokeze kupata usajili kisheria ili kazi zao ziwe salama.

Mbali na hilo Kasera alitoa wito kwa wabunifu ambao wamesajili bunifu zao kuendelea kuziboresha kulingana na mahitaji ya jamii ili ziwe na tija kwao na taifa kwa ujumla.

"Kwa zile bunifu zilizosajiliwa maendeleo endelevu wanajaribu kuziboresha kwa kadri mahitaji ya jamii yanavyohitaji. Tangu mwaka 2019, China inaongoza kwa kutoa bunifu nyingi lakini haiongozi kwa kutoa ubunifu mpya bali inaongoza kwa kuziongezea ubora kazi za ubunifu za zamani,"alisema

"Kwa mfano ubunifu wa gari. Miaka yote gari lipo lakini siku zinavyokwenda wanatoa matoleo mapya yenye ubora zaidi, ulinzi na uharaka, hivyo BRELA tumekuwa tukitoa elimu ya namna gani wanaweza wakaboresha zile kazi za ubunifu ambazo zimesajiliwa" alisema

Hata hivyo alisema BRELA inaangalia namna ambayo wanaweza kushirikisha taasisi zingine katika kusaidia kuzipatia soko kwa bunifu hizo.

Alisema unakuta mtu ana ubunifu mzuri lakini hawezi kuzipatia soko kwa hiyo BRELA na taasisi zingine za kikanda na kimataifa wamekuwa wakiangalia zinahitaji msaada upi ili kuzitafutia soko.

Kasera alisema BRELA itaendelea kupita kwenye mabanda na kuzungumza nao kuwa hii inaweza kupata ulinzi au kuongeza ubora wa bunifu zao.

# Mpango: Bila utafiti ni vigumu kupata mafanikio katika kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema bila kufanya utafiti kwenye kilimo itakuwa vigumu kufanikiwa.

Pia ameitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuangalia namna ya kutoa mikopo ya elimu ya juu ya upendeleo kwa wanafunzi wanaosoma sayansi, teknolojia na ubunifu.

Dk. Mpango aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye kilele cha Wiki ya Ubunifu kilichoambatana na utoaji tuzo kwa washindi wa Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) mwaka 2022.

Aliwataka watafiti kufanya utafiti wa mbegu zinazohimili mazingira magumu ili ziwasaidie wakulima.

"Nyinyi watafiti wetu mtusaidie sana wananchi wa Dodoma wapo kwenye mazingira ambayo mvua ni kidogo sana lakini ardhi ya Dodoma ni nzuri sana. Lazima mtusaidie kutambua mazao ambayo yanaweza kulimwa Dodoma na kumuinua mkulima wa chini. Mimi naweza kukupeleka eneo ambalo nalima na parachichi zimekubali vizuri kwa Dodoma," alisema.

Alisema kuna mazao yakilimwa kwenye mkoa husika yatamwinua mkulima.

Kuhusu ubunifu, Dk. Mpango alitaka kuwafuatilia na kuwatambua vijana na watoto wenye vipaji vya ubunifu nchini kote na kuwasaidia sambamba na kuwapa fursa za kueleza ndoto na ubunifu wao.

"Mshirikiane na sekta binafsi nchini kueleza vivutio vya kuwatia hamasa wanasayansi, wahandisi na wataalam wa tiba waweze kufanya tafiti, bunifu kwa ari zaidi," alisema.

Aliagiza Wizara ya Elimu kupanua na kuboresha elimu ya ufundi nchini na kuhakikisha kuwa elimu hiyo inamfanya mhitimu aajirike kwa wepesi.

"Takwimu za mwaka 2020 zinaonyesha kuwa maombi ya hatimiliki kutoka Tanzania yaliyowasilishwa katika Shirika la Hatimiliki la Dunia ni 97 lakini Kenya iliwasilisha maombi 459 wakati Afrika Kusini iliwasilisha maombi 7,603. Idadi hiyo ya maombi ya hatimiliki kutoka Tanzania ni ndogo sana ukilinganisha na idadi kubwa ya watafiti tulio nao ambayo nimewashuhudia hivi punde,"alisema.

Makamu wa Rais aliitaka Wizara kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha halmashauri zinatenga maeneo maalumu ya ubunifu na atamizi kwa wabunifu wa kisekta kulingana na shughuli za kiuchumi ili kulea vijana wenye ubunifu.

Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, aliwaahidi wabunifu serikali kuwahudumia ili kuhakikisha ubinifu unakuwa na manufaa kwa jamii huku akizitaka taasisi zinazohudumia wabunifu kujipanga kwa kuwasaidia wabunifu.

Naye Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali imeanzisha zaidi ya kumbi 50 za ubunifu na teknolojia nchini kwa ajili ya kuendeleza wabunifu wachanga.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNDP), Christine Musisi, alipongeza Tanzania kwa kuweka suala la ubunifu katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano.





# Wageni wachangamkia uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema nchi nyingi zimeonyesha nia ya kuunga mkono serikali katika utekelezaji wa sera ya uchumi wa bluu kupitia mpango wake wa matumizi ya bahari.

Aliyasema hayo mjini Zanzibar wakati akifungua kongamano lililoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi lililowashirikisha wadau wa maendeleo ya uchumi wa bluu na serikali pamoja na sekta binafsi, kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya uchumi wa bluu.

Suleiman alisema Zanzibar inaendelea kutekeleza miradi inayohusu sekta ya uchumi wa bluu ikiwamo ujenzi wa soko la kisasa na viwanda vya kukaushia samaki na kusarifu mitambo ya barafu chini ya ufadhili wa Korea pamoja na kununua boti kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi wadogo.

Akizungumzia utunzaji wa mazingira ya bahari, alisema bahari ni moja ya rasilimali muhimu iwapo itatumika vizuri, hivyo ni vyema wadau mbalimbali wa uvuvi kuwaelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira ya bahari ili kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kupitia mazao ya baharini.

Naye Naibu Mwakilishi wa UNDP Tanzania, Sergio Valdin, alisema UNDP inaendelea kuiunga mkono serikali ya Zanzibar katika mahitaji ya kifedha kwa lengo la kutekeleza vipaumbele ambavyo vimo katika sera ya uchumi wa bluu ili kufanikisha azma ya serikali ya kuuendeleza uchumi wa bluu kwa vitendo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Aboud Suleiman Jumbe, alisema mkutano huo ni awamu ya tatu katika utekelezaji wa mahitaji ya kifedha ambapo kwa sasa kwa kipindi hiki cha miaka mitano wanatarajia kupata dola bilioni 179 ambazo zitatumika katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini.

Alisema sekta ya uvuvi na mazao ya baharini ni moja wapo ya sekta muhimu na kubwa ambayo ina mafanikio na kuleta maendeleo makubwa kwa nchi na wananchi kwa ujumla.

Mtaalamu wa Miradi wa UNDP Tanzania, Abbas Kitogo, alisema UNDP inashirikiana na serikali katika kufanikisha vipaumbele vyake ikiwamo uchumi wa buluu ili kuhakikisha kuna sera imara na mikakati ambayo inadhamiria katika kufanikisha azma ya uchumi wa bluu na matumizi endelevu ya rasilimali zilizomo ndani ya bahari.




Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabani, akibadilishana mawazo na Waziri wa Elimu, Lela Mohamed Mussa, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Waziri ataja manufaa matumizi mfumo wa TEHAMA bandarini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema uwekaji wa matumizi ya mifumo ya kisasa katika Shirika la Bandari Zanzibar utasaidia kuleta mabadiliko ya kiutendaji na kuondosha upotevu wa mapato ya serikali.

Dk. Khalid aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati akizindua mradi wa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa bandari ya Malindi Unguja.

Alisema kuwapo kwa mfumo huo, kutarahisisha kukuza utoaji wa huduma ndani ya shirika hilo na kuimarisha mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato.

Waziri alisema anaamini katika kipindi kifupi kijacho, ndani ya bandari ya Malindi Zanzibar huduma zitakazotolewa zitakuwa zenye ubora ambazo zitakidhi mahitaji ya wadau wote na ufanisi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto zinazokwaza upatikanaji wa huduma kwa wakati na kuondoa malalamiko kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaotumia bandari hiyo.

"Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu uwezo mdogo wa bandari katika kuhudumia wananchi hasa katika kutoa na kuingiza mizigo, hivyo mabadiliko ya mfumo wa TEHAMA yatasaidia kutoa mizigo inayoingia bandari kwa wakati," alisema.

Dk. Khalid alibainisha kwamba kupitia mfumo huo, kutawezesha kutambua taarifa za muda wa kuwasili meli pamoja na aina ya mizigo itakayowasili au kutoka.

Aliongeza kwamba utekelezaji huo utakuwa ni pamoja na kufanyika malipo kabisa ili meli inapoingia bandarini kuchukua muda mfupi kushushwa mizigo iliyobeba.

"Utoaji wa mizigo utakuwa unafanywa kwa kwa njia ya mtandao jambo ambalo litasaidia kupunguza muda wa utoaji huduma za mizigo," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Nahaat Mohammed Mahfoudh, alisema matarajio ya shirika ni kutoa huduma ili kuongeza faida kwa mujibu wa malengo ya serikali ambapo hatua hiyo haiwezi kufikiwa pasipo na mfumo wa matumizi ya teknolojia hiyo.

Alisema kupitia mfumo huo shirika hilo linatarajia kukusanya wastani wa shilingi bilioni tisa kwa mwezi kutoka wastani wa Sh. bilioni 3.5 kwa mwezi.

Mwakilishi wa ubalozi wa Finland Tanzania, Susan KaparaRo, alisema Zanzibar imeonyesha nia ya kuleta mabadiliko kwa kutumia mifumo ya teknolojia katika utoaji wa huduma ndani ya shirika la bandari jambo ambalo litasaidia kuleta mageuzi ya kiutendaji.

# Wajumbe watolewa hofu jengo la kihistoria Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, amewatoa wasiwasi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu jengo la kihistoria la Beit-al-Jaib ambalo litafanyiwa ukarabati mkubwa kwa sababu limebeba historia ya Zanzibar na ndio utambulisho wa Mji Mkongwe.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Simai alisema serikali ya Oman imeahidi kufanya ukarabati wa jengo hilo ambalo limejengwa mwaka 1883 chini ya mtawala Sultani Said Barghash kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Alisema Oman imekubali kulifanyia ukarabati jengo lingine la People's Palace lililoko Forodhani ambalo lilikuwa makazi ya watawala mbalimbali waliotawala Zanzibar.

Kwa sasa, alisema kazi inayofanyika ni kufanya upembuzi yakinifu kuhusu utekelezaji wa mradi huo ikiwamo kutafuta makandarasi watakaofanya ukarabati mkubwa.

"Mheshimiwa Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba ujenzi wa jengo la Beit-al-Jaib uko pale pale chini ya ufadhili wa serikali ya Oman ambayo imekubali pia kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la People's Palace ambalo lilikuwa la kasri la Wafalme," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya wizara hiyo, walisikitishwa na serikali kushindwa kutenga fedha kwa ajili ya kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Beit-al-Jaib na kusubiri ufadhili chini ya serikali ya Oman.

Aidha, Waziri Simai alisema katika mikakati ya kuimarisha sekta ya utalii nchini, wizara iko katika mchakato wa kuipitia Sheria ya Utalii Zanzibar Na. 6 ya mwaka 2009 kwa ajili ya kuleta ufanisi wa maendeleo ya sekta hiyo.

Aliyataja baadhi ya mambo ambayo yatapewa kipaumbele na kuangaliwa kwa kina katika mchakato wa sheria ya utalii ni pamoja na kuona sekta hiyo inawashirikisha zaidi wadau wa ndani na kimataifa katika uendeshaji wake.

## HOTUBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI



MHE. NAPE NNAUYE
**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23



MHE. MHANDISI KUNDO ANDREA MATHEW
**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**



DKT. JIM YONAZI
**KATIBU MKUU WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

**Mei, 2022**
**DODOMA**



MOHAMMED KHAMIS ABDULLA
**NAIBU KATIBU MKUU WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akishuhudia Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Mpango akipokea Bango lenye Anwani ya Makazi ya Ofisi ya Rais, Ikulu katika ukumbi wa Mkutano wa Jakaya Kikwete Convention Centre Jijini Dodoma**



# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**A. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,**
Kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

***Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye kumbukumbu za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.***

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa saba wa Bunge la kumi na mbili.

**Mheshimiwa Spika,**
Kabla ya yote, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya mwaka mmoja ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa katika sekta zote zinazogusa Maendeleo ya watu nchini.

Kwa hakika katika kipindi cha Mwaka mmoja wa uongozi wake kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonyesha Uzalendo, Uwezo, Ujasiri, Uhodari na Mapenzi yake makubwa kwa nchi yetu na wananchi wake.Hatua kadhaa za kisera na kiutendaji alizochukua katika kipindi kifupi cha uongozi wake zimekuwa na mwangwi mkubwa uliopeleka Matumaini kwa waliokata tamaa,umepeleka upendo mahali palipo nyemelewa na chuki, umepeleka heshima mahali paliponyemelewa na dharau.

Utendaji huu uliotukuka umezigusa pia sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na wadau wake. Mheshimiwa Rais kwa makusudi tarehe 12 Septemba 2021 akaanzisha wizara inayojitegemea kwa ajili ya kushughulikia sekta za Habari,Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,Muundo ambao umeongeza ufanisi katika kuzihudumia sekta husika.

Wizara inatambua matarajio makubwa waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za Habari na Mawasiliano kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara hii ndio inayosimamia Mapinduzi ya Kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika uchumi wa kidigitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na muingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidigitili. Mapinduzi haya yanawezeshwa na misingi muhimu ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Mifumo ya Mawasiliano.

Mifumo hii imerahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi zikiwemo utunzaji, utumaji na upokeaji wa fedha (Financial Inclusion), usambazaji wa bidhaa, uwepo wa vyombo vya kisasa vya upashanaji Habari pamoja na uimara wa uhuru husika. Aidha, Uchumi wa Kidigitali unawekewa mazingira bora ya Kiudhibiti, kiuwekezaji na atamizi kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa Kampuni changa za ubunifu (Startups).

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari, kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, kuendeleza wataalam wa TEHAMA, Kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Mawasiliano nchini.

Utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika katika kushiriki uchumi wa kidijitali katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) yanayowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA na pia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kama Mheshimiwa Rais alivyobainisha kwenye Hotuba yake aliyotoa hapa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

**Mheshimiwa Spika,**
Ninaomba nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuongoza Bunge la 12. Ninapenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na ya mwananchi mmoja mmoja.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika kuharakisha utoaji huduma, kufanya biashara, uzalishaji viwandani na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kujiletea maendeleo binafsi na ya Taifa kwa ujumla.

Aidha, kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara hii. Naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu; nawashukuru wadau mbalimbali kwa ushrikiano wao wakati wa kutimiza kazi zangu, bila kuisahau familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upekee niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki. Wizara imenufaika sana na umahiri, uzoefu, umakini na ushirikiano wa Kamati hii katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara.Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali wakiwemo aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu kwa tiketi ya CCM Elias John Kwandikwa, aliyekuwa
Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kwa tiketi ya CCM William Ole Nasha, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ACT -Wazalendo, Khatib Said Haji na ailyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CCM, Mkoa wa Rukwa, Irene Alex Ndyamkama. Ninaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara inasimamia Taasisi Nane zilizogawanyika kwenye umahsusi wa Huduma, udhibiti, mfuko, mashirika ya kibiashara na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); Tume ya TEHAMA (ICTC); na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC). Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi inazosimamia.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

**Ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,**
Kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2020, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 8.4 mwaka 2020. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zitolewazo na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara, Mwaka 2021 asilimia 69 ya ardhi ya Tanzania inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani.

**Mheshimiwa Spika,**
Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zinaonyesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka 52,965,816 Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia laini 55,365,239 Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka Milioni 29.1 Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia Milioni 29.9 Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka 27,326,938 Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia 35,749,298 mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Aidha, Watoa huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano wamefikia 23 ukilinganisha na watoa huduma 19 Mwezi Aprili, 2021 (hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21.1).

Watoa huduma wa huduma za ziada (Application Services and Value Added Services) wamefikia 102 ukilinganisha na watoa huduma 66 Mwezi Aprili, 2021 (ongezeko la asilimia 54.5). Pia, Bei ya mwingiliano kati ya watoa huduma (Voice interconnection Charges) imeshuka kutoka Shilingi 2.6 kwa dakika mwaka 2021 hadi Shilingi 2.0 kwa dakika mwaka 2022 (punguzo la asilimia 23.1). Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 200 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 210 Mwezi Aprili, 2022 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 50 mwaka 2021 na kufikia vituo 56 Mwezi Aprili, 2022.

Cable Television zimeongezeka kutoka 40 Mwezi Aprili, 2021 na kufikia 59 Mwezi Aprili, 2022 na magazeti yameongezeka kutoka 272 na kufikia 284 Mwezi Aprili, 2022. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za Utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 televisheni mtandao zimeongezeka kutoka 552 hadi 663 sawa na ongezeko la asilimia 20.1, blogu zimeongezeka kutoka 134 hadi 148 sawa na ongezeko la asilimia 10.4 na redio mtandao zimeongezeka kutoka 25 hadi 27 sawa na ongezeko la asilimia 8.0.

**Mheshimiwa Spika,**
Takwimu za mwezi Aprili, 2022, zinaonesha kuwa asilimia 95 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za simu za sauti na jumbe fupi, yaani 2G network kupitia minara 12,228. Aidha, asilimia 68 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye Mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za intaneti ya kasi ya 3G kupitia minara 11,753 na asilimia 45 wapo kwenye maeneo yenye Mtandao wa 4G kupitia Minara 6,656.

Hata hivyo pamoja na kwamba asilimia 68 wapo kwenye maeneo yenye huduma ya intaneti, ni asilimia 27 tu ya watumiaji wa huduma za mawasiliano wenye simu janja au vifaa vingine vya mawasiliano (laptop, tablets, iPad, n.k.) vyenye uwezo wa kutumia intaneti. Jitihada za serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya simu katika mwaka wa fedha 2021/22, pamoja na watoa huduma kutengeneza taratibu mbalimbali za kuwakopesha wateja wao simu kumeongeza idadi ya simu janja kwa takribani asilimia 2 tu kulinganisha na mwaka uliopita.

Matumizi ya TEHAMA pamoja na teknolojia zinazoibukia kama Artificial Intelligence (AI), Internet of Things (IoT), Blockchain na nyinginezo yanawezesha ujenzi wa miji ya kisasa na endelevu. Haya yote yanahitaji miundombinu thabiti na intaneti ya kasi. Upatikanaji na utumiaji wa huduma ya intaneti ya 4G kwa wananchi wengi unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa kidigiti. Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma/wawekezaji kujenga Miundombinu ya Mawasiliano ya Intanenti ya kasi ili kuongeza wigo (coverage) wa mitandao na kuimarisha ubora wa huduma za Mawasiliano ili kufikisha intaneti ya kasi kwa asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na uwezo wa kuridhisha wa Intaneti ya 4G na uwekezaji unaondelea, Serikali kupitia TCRA imeshachukua hatua za kutengeneza Mkakati wa kuchochea miundombinu inayowezesha intaneti ya kasi ya 5G. Mkakati huu unahusisha pamoja na mambo mengine kupanga na kuweka masafa yatakayowezesha uwekezaji kwenye mitandao ya 5G. Serikali kupitia TCRA ipo tayari kutoa Masafa kwa watoa huduma ambao wangependa kufanya majaribio ya teknolojia ya 5G (5G Trials). Utaratibu wa kugawa masafa yaliyobainishwa kutumika kwa teknolojia ya 5G utakuwa wa ushindani (Transparent &

# HOTUBA

Competitive Process).

**Ukusanyaji wa Mapato**

**Mheshimiwa Spika,**
Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 41,098,538,762.15 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambayo ni sawa na asilimia 82.2 ya makadirio ya makusanyo ya Shilingi bilioni 50; na kiasi cha Shilingi 8,621,793,488 kutokana na tozo ya kuongeza salio kwenye laini za simu sawa na asilimia 2.2 ya lengo la Shilingi bilioni 446.3.
Aidha, Idara ya Habari-MAELEZO imekusanya Shilingi 354,190,750 kutokana na mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi na picha ya Baba wa Taifa, vitambulisho, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti sawa na
asilimia 199 ya lengo la Shilingi milioni 178.02. Kuvuka kwa malengo ya makusanyo kumetokana na kuuzwa kwa wingi kwa picha za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuapishwa.

**Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge Mwaka wa Fedha 2021/22**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shilingi 246,384,551,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 4,984,770,000 iliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 241,399,781,000 iliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Idara ya Habari - MAELEZO na Taasisi za TBC na TSN ilikuwa imetengewa bajeti ya jumla ya Shilingi 23,744,630,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ambapo Shilingi 17,743,630,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 6,001,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika,**
Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara imepokea na kutumia jumla ya Shilingi 6,947,838,745.79 sawa na asilimia 84 ya fedha zilizotengwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa Shilingi 2,288,345,600.00 ni za Mishahara na Shilingi 4,659,493,145.79 ni Matumizi Mengineyo.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,**
Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) imepokea jumla ya Shilingi 129,713,798,179.86 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni asilimia 53.7 ya fedha zilizotengwa.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa Mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini na mijini kusiko na mvuto kibiashara. Hadi sasa utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali ambapo ujenzi wa minara 181 (passive part) umekamilika na kwa sasa hivi watoa huduma wapo katika hatua za kuagiza vifaa vya kurushia mawimbi ya simu na hatimaye kuwashwa kwa minara hiyo. Minara hii inategemewa kuwashwa kabla ya mwezi Oktoba 2022.

**Mheshimiwa Spika,**
Serikali kupitia UCSAF imengia makubaliano na watoa huduma za mawasiliano kwa ajili ya kujenga minara 161 Tanzania Bara na Visiwani. Minara hii itajengwa katika maeneo ya mipakani, Maeneo ya Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo zilikuwa hazina huduma za mawasiliano pamoja na Zanzibar. Ujenzi wa minara hii upo katika hatua mbalimbali. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi wa minara 42 upo katika hatua za ukamilshwaji ambapo ujenzi wa minara hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022. Kwa upande wa miradi mingine 119 ujenzi ipo katika hatua za awali ikiwa ni pamoja na kutafuta maeneo kwa ajili ya ujenzi pamoja na kutafuta wakandarasi. Utekelezaji wa majukumu katika maeneo mengine ni kama ifuatavyo:

**Eneo la Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara katika Eneo la Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:
i. Kuanza maandalizi ya kuhuisha Sera ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA.
ii. Kuendelea kuratibu ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta la Afrika (Pan Africa Postal Union – PAPU) jijini Arusha lenye urefu wa ghorofa 18. Ujenzi wa jengo kwa ujumla wake umefikia asilimia 65;
iii. Kuendeleza mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa ambapo Wizara imeshiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) uliofanyika tarehe 9 – 27 Agosti, 2021 Abidjan, Ivory Coast; ambapo chaguzi mbalimbali za viongozi na Mabaraza zilifanyika na Tanzania kufanikiwa kushinda nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Utawala ; na Baraza la Uendeshaji la Posta kwa kipindi cha miaka minne (2021 - 2025). Sambamba na hilo, Tanzania imepata nafasi ya Kuongoza Kamati ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao ya Umoja wa Posta Duniani.
iv. Kuendelea kuratibu jitihada za ufikishaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na yenye mawasiliano hafifu. Masuala yaliyofanyika ni pamoja na: ukaguzi wa hali ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Pori Tengefu la Loliondo lenye kata 15, visiwa 171 vya Ziwa Victoria, maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Juu Kusini, Kanda ya Kati na Pwani. Maeneo yaliyobainishwa yatafikishiwa huduma kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Aidha, katika kuratibu jitihada hizi za ufikishaji wa huduma za mawasiliano, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuimarisha Mawasiliano wa kipindi cha miaka minne (2021/22 - 2024/25) ili kuboresha huduma za mawasiliano nchini.
v. Kufanya mapitio ya sekta ndogo ya utangazaji na mfumo wa leseni ili kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sekta..
vi. Wizara imetoa leseni 25 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kupitia Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA.

**Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo:-
i. Kukamilisha uaandaaji wa Mkakati wa Taifa wa intaneti yenye kasi (National broadband Strategy);
ii. Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kushughulikia masuala ya uhalifu wa mtandao unaoongeza uratibu wa pamoja kwa taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya uhalifu wa kimtandao.
iii. Kuingia Mkataba wa Mashirikiano na TANESCO kwa ajili ya kufanya kazi pamoja ya kupitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye nguzo za umeme kwa lengo la kuongeza mtandao wa mawasiliano na wa umeme. Hatua hii imepunguza gharama za ujenzi wa Mkongo na kuharakisha mradi huu ambapo zilikuwa zijengwe Kilomita 1,880 lakini kutokana na Mkataba huu zitajengwa Kilomita 4,442 na kufikisha jumla ya Kilomita 12,761 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.
iv. Kuratibu utengenezaji wa Mfumo wa kutunza na kuchakata taarifa za kesi na matukio ya uhalifu wa usalama mtandao "cybercrimes module" inayowezesha matukio ya uhalifu kutunzwa na kufuatilia mwenendo wa mashtaka husika hadi kukamilika wake;
v. Kutoa Mafunzo kwa Waendesha Mashtaka, Wachunguzi na Wapelelezi 197 pamoja na mafunzo ya kutumia "cybercrimes module" kwa watumishi 470 wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
vi. Kukamilisha uandaaji wa rasimu ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Strategic Framework) kwa ajili ya kuchochea matumizi ya TEHAMA kwenye sekta zote za uchumi;
vii. Kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mageuzi ya Kidijitali (Digital Transformation Guideline) kwa ajili ya kutoa mwongozo wa Taasisi zote nchini wa kuelekea uchumi wa kidijitali;
viii. Kukamilisha uandaaji wa Programu ya Mafunzo ya TEHAMA yatakayopelekea kuongeza ujuzi na ubobezi wa wataalamu wa ndani ili kuendana na mahitaji ya sasa ya Uchumi wa Kidijitali;
ix. Ukamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu kwa Umma wa Usalama Mtandao (National Cyber Security Communication Strategy), 2021/22 – 2024/25; na
x. Kukamilisha na kuingia Makubaliano ya Ushirikiano kwenye maeneo ya TEHAMA na nchi ya Rwanda. Aidha, majadiliano na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Kenya, Marekani, Ujerumani, Uturuki na Falme za Kiarabu yanaendelea.
Xi. Kuanza mchakato wa kuhamishia shughuli za ujenzi,usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa Shirika la Mawasiliano la Taifa (TTCL).

**Eneo la Habari-MAELEZO**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo:-
i. Kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali. Jumla ya taarifa 18 zimetolewa kupitia vyombo vya habari.
ii. Kuratibu ratiba za Mawaziri na Viongozi kuzungumza kupitia Runinga na pia kukutana na Waandishi wa Habari kuelezea mafanikio na utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita katika Wizara zao.
iii. Kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 5,000 za Jarida la Nchi Yetu lenye kuelezea mafanikio na utekelezaji wa mwaka immoja wa Serikali ya Awamu ya Sita tangu iingie madarakani tarehe 19 Machi, 2021. Kutokana na mahitaji ya toleo hili kuwa makubwa, Wizara imechapisha nakala nyingine 10,000 na kuzisambaza katika ofisi mbalimbali za Serikali, Sekta binafsi pamoja na kuwapatia wananchi;
iv. Kukusanya na kusambaza habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya Serikali, ambapo Jumla ya habari 3,411, Makala 37, habari picha 529 katika magazeti, habari 49 katika Runinga, habari 1,600 katika "blogs" na mitandao ya kijamii zilichapishwa na kutangazwa;
v. Kuendelea kuhamasisha Vyombo vya Habari vya Nje ya nchi kuitangaza Tanzania ambapo vyombo vya habari vya nje vikiwemo CCTV, DW, BBC, Voice of Amerika, Xinhua na CGTV vilishiriki katika kuitangaza Tanzania na shughuli za utekelezaji wa Serikali;
vi. Katika kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari; Serikali imetoa jumla ya leseni mpya 19 kwa magazeti hivyo kufanya Jumla ya vyombo vya Habari vilivyosajiliwa kufikia 285.
vii. Kuhuisha Kanuni za Utangazaji kwa njia ya Kidijitali za Mwaka 2018 ili kuruhusu watoa huduma wanaotoa maudhui ya bila malipo kwa wananchi (Free to Air – FTA) kubebwa katika visimbuzi vya kulipia; na
viii. Kuendelea kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano (National Communication Strategy – NCS).
ix. Kuratibu Mkutano wa siku ya Uhuru wa vyombo vya habari Duniani ambao kwa Afrika ulifanyikia jijini Arusha Tanzania.

**Utekelezaji wa Masuala Mengine**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:
ix. Kuhuisha sheria tatu (3) na Kanuni nne (4) za Sekta; sheria zilizohuishwa ni Sheria ya EPOCA ya Mwaka 2010; Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ya Mwaka 2006; na Sheria ya Posta ya Mwaka 1993. Sheria hizi zimehuishwa ili kuboresha utendaji wa Taasisi husika na mazingira ya huduma za mawasiliano. Kanuni zilizohuishwa ni Kanuni za Leseni za Mwaka 2018; Kanuni za Utangazaji Kidijitali za Mwaka 2018; Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni za Mwaka 2020; na Kanuni za Utangazaji Redioni na kwenye Runinga.
x. Kuratibu na kusimamia uandaaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri za kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Personal Data protection) na Sheria ya TEHAMA na kuhuisha Sheria ya Huduma ya Habari;
xi. Kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26) kujumuiasha Idara ya Habari-MAELEZO;
xii. Kuajiri Mtumishi mmoja (1), kupandisha vyeo watumishi 46, kufanyika uhamisho wa watumishi 27 kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali. Aidha, Muundo mpya wa Wizara umeandaliwa baada ya kuanzishwa kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
xiii. Kuandaa Mpango wa vihatarishi wa Wizara na rejesta ya vihatarishi (risk register) na Mafunzo ya vihatarishi kwa watumishi wote wa Wizara yametolewa;
xiv. Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi tatu (3) ambazo ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Tume ya TEHAMA, na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) zimeteuliwa; na
xv. Usimamizi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara – Mtumba, lenye ghorofa saba ambapo hivi sasa lipo katika hatua ya ghorofa ya kwanza.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**
Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekusudiwa kupanua mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi zinazotuzunguka katika kufanikisha mapinduzi ya kidijitali. Katika kipindi kinachoishia Mwezi Aprili, 2022 kazi zifuatazo zimefanyika:
i. Kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Kilomita 265 (Itigi – Manyoni - Rungwa);
ii. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa kuunganisha Ofisi za Serikali (Kikombo – Mtumba – Msalato);
iii. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa Taifa kwenye eneo la Mtambaswala kuunganisha Tanzania na Msumbiji;
iv. Kukamilika kwa Upembuzi yakinifu kuunganisha Mkongo wa Taifa na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na nyaraka ya zabuni zimeandaliwa;
v. Kukamilika kwa kazi ya kukarabati Kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya TANESCO;

vi. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Huduma za Mkongo wa Taifa kwenye Mji wa Serikali Mtumba;
vii. Kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kuwezesha ujenzi wa Kilomita 4,442 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kiwango cha 200G hadi 800G na kujenga vituo vipya 37 na upanuzi wa vituo 75 vya kutolea huduma za Mkongo ambapo mikataba 22 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 141 imesainiwa. Aidha, utekelezaji huu utafikisha Mkongo katika Wilaya 23 nchini.
viii. Kukamilika kwa Upanuzi wa Mkongo wa Taifa kwenye vituo 5 vya Kigoma, Arusha, Babati, Tunduma na Mbeya vyenye jumla ya kadi za kuchakata huduma (line processing cards) 30; na
ix. Kukamilika kwa kazi ya kuhamisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa Mita 250 eneo la Mkazi – Katavi kutokana na kujengwa kwenye eneo la makazi ya watu.

**Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi**

**Mheshimiwa Spika,**
Kufuatia malengo ya Serikali ya kukamilisha Anwani za Makazi kabla ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Mwezi Agosti, 2022, katika Kikao kazi cha Wakuu wa Mikoa kilichofanyika tarehe 08 Februari, 2022; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alielekeza Mfumo wa Anwani za Makazi kutekelezwa kwa Mfumo wa Operesheni, aliyoipa jina la "OPERESHENI ANWANI ZA MAKAZI". Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimeendelea na utekelezaji wa Mradi chini uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.
Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuunda Programu Tumizi (Mobile application) ya Mfumo iliyoongeza ufanisi katika matumizi na utekelezaji wa Mfumo. Programu Tumizi imetumika katika kukusanya taarifa za barabara/ mitaa/ njia, makazi na wakazi sambamba na kumuongoza mtu kutoka anwani ya makazi moja kwenda anwani ya makazi nyingine;
ii. Semina ya kujenga uelewa kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi imetolewa kwa Viongozi 483 ambao ni Wakuu wa Mikoa; Katibu Tawala wa Mikoa; Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri; na Wajumbe wa ALAT; sambamba na Wataalam 616 wa Mikoa na Halmashauri
iii. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya anwani za makazi 12,171,320 zimekusanywa na kuingizwa kwenye Programu Tumizi. Idadi ya Anwani zilizokusanywa ni asilimia 104.3 ya lengo la jumla ya Anwani 11,676,891 zilizopangwa kukusanywa katika Mikoa yote nchini.

**Mradi wa Tanzania ya Kidijitali**

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi wa Tanzania ya Kidigitali una thamani ya Dola za Marekani Milioni 150 na ulisainiwa rasmi tarehe 19 Agosti, 2021. Mradi huu unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kuweza kufikisha huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa Wananchi. Vilevile, mradi huu unalenga kuboresha ubunifu pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini.

**Kazi zilizotekelezwa ni:-**
i. Ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mradi katika eneo la Area D na kuanza kutumika rasmi tarehe 01 Oktoba, 2021;
ii. Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji ya kuwezesha ununuzi wa bando la intaneti ya Serikali (Government internet bandwidth) kwa ajili ya matumizi ya Taasisi za Umma;
iii. Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji kuwezesha kujenga na kuboresha Mtandao wa TEHAMA unaounganisha Taasisi za Serikali (GovNET);
iv. Kukamilisha ukusanyaji wa mahitaji kuwezesha kujenga na kupandisha hadhi minara 150 ya mawasiliano kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G/4G ili kuwezesha huduma za intaneti yenye kasi kwenye maeneo hayo;
v. Kukamilisha manunuzi ya vifaa na programu endeshi za kuboresha vituo mahiri vya kuhifadhia Data (National Internet Data Centre - NIDC na Government Data Centre);
vi. Kufanya tathmini ya maeneo ya kujengewa uwezo kwa watumishi wa TEHAMA Serikalini ambapo jumla ya watumishi 450 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu; na
vii. Kufanya maandalizi ya kuwezesha ujenzi wa Chuo cha TEHAMA ambapo eneo lenye ukubwa wa Hekta 400 limepatikana eneo la Nala, Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,**
Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari umeainishwa katika Ukurasa wa 27 hadi 63 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**Makadirio ya Mapato ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 150,700,000,000 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo itokanayo na kuongeza salio la simu, usajili wa Magazeti, ada ya mwaka ya Magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

**MALENGO YA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**Mheshimiwa Spika,**
Kama nilivyoeleza awali, Wizara yangu inasimamia Mapinduzi ya Kidijitali na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka Msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Ili kuwezesha mageuzi na mapinduzi haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara imepenga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi haya ikiwemo kuharakisha uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya TEHAMA, Mawasiliano, Posta na Habari kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, anwani za makazi, mitambo ya utangazaji na Posta.

Vilevile, kufanya mapinduzi kwenye Taasisi za Sekta; kuimarisha mashirikiano na Sekta binafsi, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, kuwajengea uwezo watumishi kuendana na mapinduzi haya, kuwezesha Sekta nyinginezo kuelekea kwenye mapinduzi haya ya kidijitali; na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari. Aidha, Wizara imekusudia kufanya mageuzi kwenye taasisi zake ikiwemo TCRA kuwa mlezi na mwezeshaji zaidi wa watoa huduma za Mawasiliano na habari. kufanya mageuzi kwenye Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Mawasiliano ili kutoa huduma zake kimapinduzi na kwa weledi.

**Eneo la Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-
i. Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997;
ii. Kukamilisha kazi ya kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na maandalizi ya Mkakati wa utekelezaji;
iii. Kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016;
iv. Kufanya mapitio ya Sheria za Kisekta na Kanuni zake;
v. Kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara;
vi. Kuimarisha ushirikiano wa Sekta Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
vii. Kusimamia uboreshaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta ili kufikia wananchi wote;
viii. Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi nchini;
ix. Kusimamia utekelezaji wa mradi wa Huduma Pamoja;
x. Kusimamia upembuzi yakinifu utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce); na
xi. Kuratibu masuala ya kukuza uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano.

**Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatarajia kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali (National Digital Economy Strategy) na kusimamia utekelezaji wake;
ii. Kuratibu na kuwezesha ujenzi wa Mfumo wa TEHAMA kuratibu utendaji kazi wa Wizara;
iii. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao (National Cyber Security Strategy);
iv. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy);
v. Kuendelea kuwaendeleza wataalamu 200 kwenye maeneo ya TEHAMA yenye uhaba wa ujuzi;
vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Miongozo ya kuimarisha masuala ya utafiti na ubunifu katika TEHAMA;
vii. Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama,
viii. Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya mawasiliano ya Kikanda na Kimataifa; na
ix. Kukamilisha mchakato wa kuhamisha ujenzi,usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL).
x. Kupitia upya utaratibu unaotumika katika usimamizi wa Data Center.

**Eneo la Habari – MAELEZO**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kukusanya taarifa na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu inazozitekeleza;
ii. Kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003 ili kuifanya iendane na mabadiliko katika Sekta ya Habari;
iii. Kufanya mapitio katika Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2017;
iv. Kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari;
v. Kusimamia utekelezaji wa Sera,Sheria na kanuni mbalimbali za Habari na Utangazaji nchini.
vi. Kuchapa nakala 12,794 za Picha za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakala 12,794 za Picha za Baba wa a Taifa Mwl. Julius K. Nyerere, nakala 4,000 za Jarida la Nchi Yetu na nakala 2,000 za Bango la Baraza la Mawaziri (Cabinet posters);
vii. Kuchapa na kutoa leseni za magazeti na vitambulisho vya waandishi wa Habari;
viii. Kutoa miongozo na kufanya tathmini ya utoaji taarifa kwa umma kwa kila Taasisi;
ix. Kuhamasisha Vyombo vya Habari vya nje ya nchi katika kuitangaza Tanzania;
x. Kuanza Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano (National Communication Strategy – NCS);
xi. Kuanzisha Kipindi Maalum cha Ongea na Waziri; na
xii. Kujenga Studio maalum kwa ajili ya Vipindi vya Moja kwa Moja vya redio na runinga.

**Miradi Itakayotekelezwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/23**

**I: Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika**
Wizara imeanza mchakato wa kuhamishia shughuli za Kujenga na kuendesha Mkongo wa taifa wa mawasiliano kwa Shirika la mawasiliano nchini TTCL. Mchakato huu utakamilika mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 149,700,000,000 ambapo Shilingi 149,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 700,000,000 ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Fedha hizi zitatumika kujenga Kilomita 1,600 za Mkongo na Vituo vipya 15 vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi kufikisha ngazi za Wilaya nchini. Ujenzi huu utawezesha kufikisha huduma za Mkongo kutoka Wilaya 81 kati ya Wilaya 139.

**Mheshimiwa Spika,**
Shughuli nyingine zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu ni:

i. Kufanya Ujenzi wa Mkongo wa majini kiasi cha Kilomita 60 kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika;
ii. Kufanya tathmini ya Ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi Data Zanzibar;
iii. Kuwajengea uwezo wataalam 150 kwenye TEHAMA;
iv. Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;
v. Kukamilisha Nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sheria ya TEHAMA na Mkataba wa Jumuiya ya Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Malabo Convention);

# HOTUBA

vi. Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni;
vii. Kuwezesha utendaji kazi wa Kamati za Kiufundi kwa ajili ya usimamizi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;
viii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa mradi; na
ix. Kuandaa Mpango Mkuu (Master Plan) wa utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**II: Mfumo wa Anwani za Makazi**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 40,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:
i. Kuhakiki miundombinu iliyowekwa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ili kuhakikisha viwango vimezingatiwa;
ii. Kuhakiki taarifa zilizokusanywa kwenye Operesheni Anwani za Makazi;
iii. Kuboresha Kanzidata na Programu Tumizi ya Mfumo;
iv. Kuendelea kuunganisha Mfumo wa Anwani za Makazi na Mifumo mingine ya kutoa huduma za kijamii;
v. Kutoa elimu kwa umma; makundi maalum ya kijamii kuhusu manufaa na matumizi sahihi ya Mfumo na kujengea uwezo Taasisi za umma na binafsi kutoa huduma kupitia Mfumo;
vi. Kutunga Sheria ndogo za kuwezesha ujenzi na matumizi ya Mfumo, mapitio ya Sheria ya EPOCA na Kanuni zake kuwezesha matumizi ya Mfumo;
vii. Kununua servers mbili (2) kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za Mfumo na vifaa vya kuwezesha matumizi ya Mfumo;

viii. Kuandaa mwongozo ya namna mpya ya kufanya biashara kwa kutumia Mfumo;
ix. Kutengeneza Mkakati wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Mfumo; na
x. Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mfumo.

**III: Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania)**

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unalenga kuleta mabadiliko ya Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy). Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo (SMEs na SMMEs); kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya Serikali na waliopo nje ya Serikali; na kuongeza uwezo wa utoaji wa Huduma za Serikali kwa kuwezesha uwepo wa intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya Serikali ili kumnufaisha mwananchi. Mradi huu utaanza kujenga chuo mahiri cha TEHAMA nchini (Digital Technology Institute). Aidha, mradi huu utapelekea Mawasiliano kwenye maeneo mapya 763 ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 111.59 kitatumika kupitia mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 39,300,000,000 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kujenga kituo kimoja (1) cha kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitano (5) kwenye kila Kanda;
ii. Kuwezesha ununuzi, ugavi na ufungaji wa vifaa katika kituo kimoja (1) kikubwa na vituo vidogo vitano (5) vya kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA;
iii. Kuwezesha ununuzi wa 'bandwidth' kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali;
iv. Kusimika mitambo kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data (NIDC);
v. Kukarabati vituo 10 vya Huduma Pamoja;
vi. Kujenga mfumo wa kitaifa utakaorahisisha ukusanyaji wa takwimu za TEHAMA;
vii. Kujenga, kupanua na kuboresha miundombinu iliyopo ya intaneti yenye kasi (broadband) inayomilikiwa na Serikali (GovNET) na kuunganisha taasisi 100 kwenye Miundombinu hiyo na kufikisha taasisi 390 zilizounganishwa;
viii. Kutekeleza programu ya uelimishaji umma kuhusu mradi;
ix. Kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua (refurbishment) vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza;
x. Kujenga minara ya mawasiliano 150 kwenye Kata 150 ili kuwezesha huduma za mawasiliano nchini;
xi. Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya TEHAMA;
xii. Kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia watalaam 200 mafunzo ya muda mfupi na wataalam 10 mafunzo ya muda mrefu; na
xiii. Kufanya tathmini ya kuainisha mahitaji ya usanifu wa kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

**IV: Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 3,300,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kujenga Kituo cha Kuendeleza Wataalam, tafiti na ubunifu wa TEHAMA na kufanya maandalizi ya ujenzi wa makao makuu ya Tume ya TEHAMA;
ii. Kukiendeleza kituo cha kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam na kujenga vituo viwili (2) vya Kanda vya kutengeneza bidhaa za TEHAMA;
iii. Kuanzisha Vituo vya Ubunifu na Atamizi TEHAMA katika Wilaya mbili (2) nchini;
iv. Kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA nchini (ICT human capital development system); na
v. Kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.

**V: Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) unalenga kuboresha upanuzi wa usikivu wa Shirika Nchi nzima. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 13,136,500,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo.

i. Upanuzi wa Usikivu redio za TBC kwenye maeneo yasiyokuwa na ausikivu nchini;
ii. Ukarabati wa ofisi, ununuzi wa Mitambo na vifaa vya utangazaji vya Chaneli ya Tanzania Safari;
iii. Kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha;
iv. Kuwezesha ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);
v. Ujenzi jengo la Makao Makuu ya TBC Dodoma na ukarabati wa majengo ya Ofisi yaliyopo;
vi. Kuwezesha ununuzi wa Magari ya kurushia matangazo mubashara ya Redio (TBCTaifa naTBCFM) na Televisheni (TBC1, TB2 na TBConline) na pia Magari kwa ajili ya Shughuli nyingine za Utangazaji;
vii. Kuwezesha ununuzi wa vifaa 18 vya kurushia Matangazo mubashara ya Redio nje ya studio;
viii. Ununuzi wa mitambo 10 na vifaa vya kurushia matangazo mubashara ya Televisheni (TBC1, TBC2 na Ofisi za Kanda);
ix. Ukarabati, uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi wa Nchi Kusini mwa Afrika katika jengo la utangazaji Barabara ya Nyerere kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya picha na sauti;
x. Ufungaji wa mifumo ya uhariri, upokeaji na urushaji wa Matangazo kupitia mifumo ya TEHAMA (Robotic Intergrated News system with international news Monitoring); na
xi. Kuwezesha ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBC Mtandaoni na televisheni ya Kiingereza ya online.

**VI: Mradi wa Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi huu unalenga kuwezesha Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kufunga mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji ambao utakuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya Kampuni. Mtambo huu unatarajiwa kuboresha mwonekano wa magazeti ya Serikali na hivyo kuvutia wasomaji na watangazaji na pia kufanya uchapaji wa kibiashara kwa bidhaa mbalimbali chapishi kwa wateja wa ndani na nje ya nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 9,400,940,000 fedha za ndani kwa ajili ya kuwezesha ufungaji wa mitambo tajwa.

**VII: Mradi wa Habari kwa Umma**

**Mheshimiwa Spika,**
Mradi huu unalenga kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali. Vilevile, mradi unakusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kupata maoni ya wananchi katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 940,940,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.
Mheshimiwa Spika,

Mipango itakayotekelezwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 imebainishwa kwa kina katika Ukurasa wa 74 hadi 84 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

**D. SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew (Mb.), Naibu Waziri; Dkt. Jim Yonazi, Katibu Mkuu na, Mohammed Khamis Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara yangu, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Habari na TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba nichukue fursa hii kwa upekee niweze kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Mawasiliano. Washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA), Ubalozi wa China nchini na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

**Mheshimiwa Spika,**
Ningependa pia kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya Kikanda yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Mawasiliano inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kwa upekee pia niwashukuru vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi yetu kwa ushirikiano mkubwa walioonyesha katika kipindi cha utekelezaji wa shughuli zetu kama Wizara. Wanahabari ni wadau muhimu katika wizara yetu. Nawashukuru kipekee kabisa kampuni zote za simu nchini, kwa kuendelea kuwekeza kwenye huduma hii, kutoa ajira, kulipa kodi na kutoa huduma za teknolojia mbalimbali katika maisha ya kila siku nchini.

**E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 282,056,786,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:-

i) Kiasi cha Shilingi 26,279,346,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi 17,249,317,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 9,030,029,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.
ii) Kiasi cha Shilingi 255,777,440,000.00 kinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 215,777,440,000.00 ni Fedha za Ndani na Shilingi 40,000,000,000.00 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni **http://www.mawasiliano.go.tz.**

***Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.***

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Unawajua waliopiga nyimbo za vipindi RTD?

**Na Adam Fungamwango**

KWA yoyote aliyezaliwa miaka ya 1990 kurudi nyumba, atakumbuka nyimbo za vipindi mbalimbali vya iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), ambayo kwa sasa ni Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC).

Wakati huo hakukuwa na televisheni, simu, mitandao ya kijamii, wala vituo vingi vya redio kama ilivyo sasa.

Ilikuwepo redio hiyo tu moja, iliyokuwa na idhaa mbili, ya taifa ya biashara.

Ndiyo maana wengi wanakumbuka kipindi mbalimbali vilivyokuwa vikirushwa kwa sababu ilikuwa ni lazima tu usikilize hata kama hupendi, labda uzime redio.

Wengi wanakumbuka kuwa redio ilikuwa inafunguliwa saa 11:00 alfajiri na kufungwa saa sita usiku.

Sasa kuanzia hiyo alfajiri kunakuwa na mlolongo wa vipindi vikianza vile ya dini vya kufungulia vipindi, na vipndi vingine kama Kumekucha, Majira, Asubuhi Njema, Mchama Mwema, Mashairi, Tumbuizo Asilia, Kijaluba, na vingine vingi.

Vyote hivyo vilikuwa na nyimbo ambazo zilitumika kufungulia au kufunga vipindi hivyo.

Hata hivyo, inawezekana mpaka leo hii si wote waliokuwa wanajua nyimbo zile ambazo zingine ziliimbwa na zingine ni la ala zilikuwa za bendi gani au mwanamuziki gani. Ukweli ni kwamba baadhi ya wanamuziki wa Tanzania, na bendi za hapa hapa, lakini zingine ni za wanamuziki kutoka nje ya nchi.

Inawezekana baadhi wanafahamu baada ya nyimbo za vipindi zilipigwa na nani, lakini si zote.

Leo tutapata kuwafahamu ni ni wanamuziki au bendi gani walipiga nyimbo za kipindi gani maarufu wakati huo RTD.



### UGUA POLE-OMARY KUNGUBAYA

"Wakati umewadiwa wa salamu za wagonjwa hospitalini leo tunawapa pole. Ajuaye Bwana Mungu kwa mzima kuwa mfu mgonjwa kuwa salama leo tunawapa pole. Kipindi chenu kinawapa pole wote tunawapa pole, Mungu atawajalieni pole, msiwe na mashaka wote pole. "

Hicho ni kipande cha wimbo uliokuwa kiashiria cha kipindi cha 'Ugua Pole' kilichokuwa kikianza mida saa 4:00 asubuhi mpaka saa 5:00 asubuhi. Ni kipindi ambacho watangazaji walikuwa wakiwatembelea wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali mbalimbali nchini, kwa namna ya kuwafariji, wakiwauliza nini kinawasibu, walianza lini kuumwa, wanajikiaje, matibabu yakoje na mwisho walikuwa wanapewa nafasi ya kuchagua wimbo.

Kipindi hicho kikiisha kuna mashairi yanabadilika na kuimbwa

"Tunawaaga nyote kwa heri, Mungu atawajalie pole, msiwe na mashaka wote pole, dakitari atatibu tena. Tunawageni wote kwaheri, wiki ijayo tuonane tena."

Huu wimbo ulipigwa na mwanamuziki aitwaye Omari Kungubaya. Alipiga wimbo huo akitumia gitaa kavu aina ya 'galatoni'.

Mwanamuziki hiyo alizaliwa 1939 na kufariki Oktoba 20 2016.

Historia yake kimuziki inaanzia mwaka wa 1955 akiwa shuleni Msamvu mkoani Morogoro, ambapo wakati huo alikuwa na umri wa miaka 16 tu, na aliweza kuchaguliwa kuwa kiongozi wa bendi ya shule na mara baada ya kumaliza shule akajiunga rasmi na bendi ya Cuban Marimba iliyokuwa chini ya Salum Abdallah Yazidu.

### TAARIFA YA HABARI-MORRIS NYUNYUSA

Sidhani kama kuna mtu hajawahi kusikia ngoma zilizokuwa zinapigwa kwenye taarifa ya habari zote kuanzia asubuhi hadi usiku. Hata sasa TBC kuna wakati wamekuwa wakipiga kipande hicho cha ngoma wakati wa taarifa ya habari.

Ngoma za kiashiria za taarifa ya habari wakati huo, zilipigwa na mzee Morris Nyunyusa aliyekuwa mlemavu wa macho.

Mzee huyo awali alikuwa na uwezo wa kupiga ngoma kumi kwa mara moja, lakini baadaye akaongeza hadi ngoma 17.

Midundo yake ikisikika tu, basi kila mtu anajua ni taarifa ya habari. Moja ya mafanikio yake makubwa kwenye kazi yake hiyo ya sanaa ni kuiwakilisha Tanzania kwenye tamasha la Expo 70, Osaka nchini Japan, ambapo pia picha yake iliwekwa mpaka kwenye stempu za Shirika la Posta wakati huo.

Midundo yake huyo ilimpatia sifa sana si ndani ya nje ya nchi. Baada ya kutoka Japan, Mbaraka Mwinshehe ambaye alikuwa mmoja wa washiriki na tamasha hilo alitunga wimbo wa 'Expo 70' na kumtaja msanii huyo.

Kwenye wimbo huo, hiki ni moja ya kipande ambacho Mbaraka anaimba "maonyesho Japan yalifana sana Likembe, Mahoka na ngoma za Taifa, wacheza midimu na wachezea nyoka, mzee Morris na ngoma zake kumi oyeee."

### KUMEKUCHA-MARIJANI RAJAB

Ni kipindi ambacho wanafunzi wengi walikuwa hawakipendi. Na wimbo wenyewe walikuwa hawataki hata kuusikia. Siyo kwamba kipindi au wimbo ulikuwa mbaya. Kipindi hicho kilikuwa kikianza saa 11:30 alfajiri na kumalizika saa 12:00 asubuhi, kipindi ambacho ndiyo walitakiwa waamke kujiandaa kwenda shule. Ilikuwa mhitani sana kuamka.

Wimbo wa kiashiria cha wimbo huo 'Kumekucha' na kipindi chenyewe kiitwa hivyo hivyo, kilipigwa na bendi ya Safari Tripers, utunzi wake Majirani Rajab.

"Kumekucha sasa kumekucha. Majogoo vijijini wanawika, hata na jua mbinguni, wazalendo amkeni tukalime sasa.." Ukisikia maneno ya kipande hicho unatakiwa uwe umeshaamka, au uamke ujiandae kwenda shule. Ujue kipindi ndiyo kinaanza. Lakini kilimalizika, mashairi nayo yanabadilika.

"Sasa kaziii ooo mama ooo sasa kazi, wacha uvivu na kazi ooo mama..." Kama bado upo nyumbani hujaondoka ukisikia mashairi hayo, ujue kipindi hicho kimeisha na tayari umeshachelewa namba shuleni, kilichobaki ujinadae na bakora tu.

### JIONI NJEMA-JAMHURI JAZZ BAND

Hiki ni kipindi ilichokuwa kikianza majira ya saa 11:00 jioni hadi saa 12:00. Kipande cha wimbo wa kipindi cha 'Jioni Njema' kilipigwa na bendi ya Jamhuri Jazz ya Tanga. Ni wimbo wa ala ambao umetokana na kibao cha 'Mganga namba moja.

### MISITU NI UHAI-JOHN KOMBA

Hiki ni kipindi kilichokuwa kikisikika majira ya saa nane, nane na nusu au tisa kasorobo. "Watanzania Bara na Visiwani, tutunze misitu ni uhai, tangu zamani tulipewa urithi, tuhifadhi mistu ni uhai haya..." Ni baadhi ya maneno yaliyopo kwenye wimbo huo wa kipindi cha 'Misitu ni Uhai'. Ulipigwa na kikundi cha Sanaa cha Jeshi la Wananchi Tanzania, na mtunzi na mwimbaji mkuu akiwa ni marehemu Kapteni John Komba ambaye baadaye aliondoka huko na kuwa kiongozi wa kundi la Tanzania One Thearte (TOT).

### MICHEZO- ALOIS MAXWELL

Kama ulikuwa hujui basi leo ndiyo utamjua mwanamuziki aliyepiga kipande cha kipindi cha 'Michezo' RTD enzi hizo. Wengi wanakumbuka hadi leo, kwani TBC imeendelea kukipiga kipande hicho hadi leo.

Aliyekitwanga ni Mmarekani Alois Maxwell Al Hirt aliyezaliwa Novemba 7, 1922 na kufariki Aprili 27, 1999 akiwa na miaka 76. Alikuwa ni mpiga ala za upepo maarufu duniani, akiuza nakala nyingi za nyimbo zake na kupata tuzo kibao. Ukisikiza kipande cha wimbo wa kipindi cha michezo 'trumpet' zimetembea sana humo, pamoja na drums. Aliyepuliza ndiyo huyo Mmarekani. Hakuna mwanamichezo yoyote wakati huo aliyekuwa akitaka kusikiza kipindi hicho saa mbili kasorobo usiku, asikijue kipande hicho cha kuashiria kipindi hicho au kumaliza.

Alifariki dunia kwa ugonjwa wa ini, akiugua kwa miaka minane, akiwa hawezi kutembea na maisha yake yaliyosalia, aliyamaliza kwa kukaa kwenye kiti cha walemavu kutokana na maradhi hayo. Alicha mke na watoto wanane.

Huyu ndiye mtu aliyepiga kipande cha wimbo uliokuwa unasikika kwenye kipindi cha 'michezo' kwenye Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), sasa ikiitwa TBC. Ni mwanamuziki mpiga 'trumpet' na ala zingine za upepo wa Kimarekani anaitwa Alois Maxwell Al Hirt aliyezaliwa Novemba 7, 1922 na kufariki Aprili 27, 1999 akiwa na miaka 76.



HABARI KIMATAIFA

## Marekani yamtetea mwigizaji wa filamu 'Hoteli Rwanda'

**WASHINGTON,** MAREKANI

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Marekani, imesema Paul Rusesabagina, ambaye filamu aliyoicheza ya Hotel Rwanda iliteuliwa katika tuzo ya Oscar alikamatwa kimakosa.

"Uamuzi huo ulizingatiwa kwa ujumla na ukosefu wa hakikisho la uhuru wa kesi yake ," alisema msemaji wa Wizara hiyo Alhamisi.

Rusesabagina alihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela na mahakama ya Rwanda mwaka jana katika kile ambacho wafuasi wake walisema ni kesi bandia.

Inasemekana aliwaokoa watu 1,200 wakati wa mauaji ya kimbari ya mwaka 1994, lakini serikali ya Rwanda ilisema hakuna uthibitisho unaoonyesha kuwa aliwaokoa watu hao.


Mwaka 2011, Rusesabagina alishutumiwa kudhamini kundi la muungano wa makundi ya ugaidi yenye silaha na itikadi kali, ambalo mwaka 2018 lilidai kufanya mashambulizi kwenye ardhi ya Rwanda kwenye maeneo ya msitu wa Nyungwe ambapo watu wengi waliuawa.

Kabla ya kufungwa Rusesabagina pia alikuwa ni Naibu kiongozi wa muungano wa vyama vya kisasa vinavyoipinga serikari ya Rwanda vyenye makundi ya kijeshi ya FLN unaoendesha harakati zake mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Familia yake ilisema inatumaini uamuzi huo mpya wa serikali ya Marekani utaongeza shinikizo kwa Rwanda kumuachilia huru Rusesabagina mwenye umri wa miaka 67.

Mwezi uliopita familia yake iliwasilisha mashitaka ya kudai fidia ya dola milioni 400 nchini Marekani kuhusu madai ya kutekwa na kuteswa.

Familia yake ilisema serikali ya Rwanda ilimlaghai kutoka Texas, ambako alikuwa akiishi uhamishoni na kumpeleka Rwanda. **BBC**



# Ukraine yaulilia mji wa Donbas, yathibitisha umeteketezwa kabisa

**KYIV,** UKRAINE

HATIMAYE Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amethibitisha kwamba mji wa Donbas, umeteketezwa kabisa na vikosi vya Russia.

Zelensky aliishutumu Russia kwa kugeuza eneo la mashariki la Donbas kuwa 'kuzimu,' huku mapigano makali yakiendelea katika sehemu mbalimbali.

Akizungumza wakati wa hotuba yake ya usiku mjini Kyiv, alisema vikosi vya Urusi vimesambaratisha eneo hilo kiasi cha kutisha.

"Kuna mashambulizi ya mara kwa mara katika eneo la Odesa, katika miji ya katikati mwa Ukraine. Donbas imeharibiwa kabisa," alisema.

Aliongeza "Haya yote hayana na hayawezi kuwa na maelezo yoyote ya kijeshi kwa Russia. Hili ni jaribio la kimakusudi na la uhalifu la kuua Waukraine wengi iwezekanavyo,".

Akizungumza kwa huzuni alisema "Endeleeni kuharibu nyumba nyingi, vituo vya kijamii na biashara kadiri inavyowezekana,"

Juzi wizara ya ulinzi ya Ukraine iliishutumu Russia kwa kuzidisha mashambulizi yake huko Donbas na kuwazuia raia kukimbia.

**KHERSON KUWA SEHEMU YA RUSSIA**

Gavana aliyewekwa madarakani na Russia katika jimbo la kusini mwa Ukraine la Kherson, amesema eneo hilo litaingizwa kuwa sehemu ya nchi hiyo.

Volodymyr Saldo, ambaye aliwekwa mamlakani na vikosi vya Russia baada ya kuchukua udhibiti wa eneo hilo mapema mwezi Machi, aliandika kwenye Telegram kwamba litakuwa jimbo la Kherson la shirikisho la Russia.

Naibu wake, Kirill Stremousov, aliandika kuwa wakazi wa jimbo hilo wataweza kuwasilisha maombi ya uraia wa Russia wiki zijazo wakati hali itakapoimarika.

Maofisa wa Ukraine walionya mara kwa mara kwamba Russia inapanga kuendesha kura ya maoni bandia katika jimbo hilo na maeneo mengine.

Hata hivyo, maofisa wa Russia bado hawajathibitisha iwapo majimbo ya kusini mwa Ukraine yamechukuliwa. Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, alisema mapema mwezi huu kwamba hali ya baadaye ya maeneo hayo itategemea utashi wa wakazi.

Marekani kusaidia makombora

kushambulia meli za kivita

Maofisa wa Marekani wanafikiria kuwasaidia wanajeshi wa Ukraine na makombora ya kushambulia meli , shirika la habari la Reuters limesema.

Ikinukuu maofisa wa serikali ya rais Biden, ripoti hiyo ilisema kwamba Ikulu ya Whitehouse huenda ikaipatia Kyiv makombora ya Boeing Harpoon na yale ya naval Strike ambayo watayatumia kulenga meli ya kijeshi ya Urusi kwa jina Black Fleet, ambayo kwa sasa ipo katika bandari za pwani ya Ukraine.

Maofisa wa Ulinzi wa Uingereza walisema kwamba takriban meli 20 za kijeshi za Russia , ikiwemo manuwari zipo katika eneo hilo.

Maofisa wanaamini kwamba silaha hizo huenda zikasaidia kuzifukuza meli za Russia kutoka katika himaya ya Ukraine na kuruhusu uuzaji wa nafaka na bidhaa nyengine za kilimo.

Lakini makombora hayo ambayo yanagharimu takriban dola milioni 1.5m kwa raundi moja na yanaweza kuruka umbali wa kilomita 300, ni ya baharini hivyo basi huenda Ukraine ikapata ugumu wa kushambulia kutoka ufukweni.

**BBC**



Meli ya kivita ya Russia ikiwa katika bahari nyeusi ikiongoza mashambulizi ya makombora dhidi ya miji ya Ukraine. **PICHA: BBC**

# Museveni akutana na Raila Odinga

**ENTEBBE,** UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amesema mazungumzo na mgombea urais wa Kenya, Raila Odinga yaliyofanyika Ikulu ya Entebbe yaligusia masuala yanayohusu nchi hizo mbili jirani.

Odinga, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa wagombea wanaoangaliwa kushinda katika uchaguzi wa urais wa Agosti 9, alimtembelea Rais Museveni juzi jioni.

Katika ujumbe wake wa Twitter kuhusu mkutano huo, Odinga alisema wamejadili historia ya pamoja ya nchi zao inayolenga kuimarisha uhusiano wa siku zijazo.

Siku mbili zilizopita, Odinga alikuwa Sudan Kusini ambako alikutana na Rais Salva Kiir na kuzindua Daraja la Uhuru la kilomita 3.6 linalotarajiwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa katika Mto Nile.

Orodha ya wagombea urais 55 wameidhinishwa kugombea katika uchaguzi wa Kenya.

Odinga anatarajiwa kukabiliwa na changamoto kubwa kutoka kwa Naibu Rais William Ruto, anayewania kupitia tiketi ya muungano wa Kenya Kwanza.

Uchaguzi wa Kenya ni muhimu katika kanda hiyo kwa sababu ndio mahali pa kuingizia bidhaa kutoka nchi zisizo na bandari kama vile Uganda, Sudan Kusini na Congo DR.

Eneo hilo litakuwa na wasiwasi kutokana na uchaguzi uliokumbwa na ghasia wa mwaka 2007 ambao uliathiri uchumi wao.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**AMAN ROBERT MPUNGU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4177-0094 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **HWAZI** mwaka 2011, na cheti cha chuo **CERTIFICATE** chenye namba ya usajili **CGA/2013/06/1525** kozi ya **GENERAL AGRICULTURE** kilichotolewa na chuo cha **MATI-TUMBI** mwaka 2015,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa MPA/B.1/20/VOL.XX/72**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMILY PAPIAN JOHN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T412BEE** aina ya **Suzuki ESCUDO**, yenye Chassis **No.TD01W217521, Engine No. G16A406328.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/198429/202**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA (W) BOMANI –IRINGA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)(R: E 2002)**
**SHAURI LA MADAI YA TALAKA 21/2022**
**MDAI: MARIAMU SAMWELI MWALUKO**
**MDAIWA: ABDALLAH JUMA**

Shauri la madai ya talaka tajwa hapo juu limefunguliwa katika mahakama hii tarehe 21/04/2022 na mdaiwa mtajwa hapo juu ,akiomba kuachana na mdaiwa.

Hivyo basi unaarifiwa wewe mdaiwa popote pale ulipo kuhudhuria hapa mahakamani siku ya 02/06/2022 saa 2:00 asubuhi bila kukosa siku hiyo kwa ajili ya kujibu madai hayo.

Na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ,ni lazima kuleta nyaraka na ushahidi wako kwa ajili yakujitetea ,usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja nakutolewa hukumu.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 18/05/2022.**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**ZAINAB MPUYIKI MGUDE** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya Honda yenye usajili namba **MC359 BUU, CHASSIS NAMBA MD201000342.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/2072/2022**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER** yenye usajili namba **MC420 BJZ, CHASSIS NAMBA MD2A21BZ1GWC85909, ENGINE NAMBA: PFZWGC30022.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/2072/20222**.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAPHAEL HENRY KAZIMOTO**

Anatangaza kupotelewa kwa Kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 821 DBF . Yeyote atakaeiyona atoe taarifa **kituo cha polisi au piga simu 0672338343**

**MOR/MOR/RB/535056/2021**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Mimi nadhani bora tu kesho niondoke Siwatu."

"Kwa nini?" Akajibu na kumtazama Bakari kwa jicho kali. Mwenyewe aligundua hilo na kuyaondoa macho yake taratibu kwa Siwatu.

"Kwa hayo uliyoniambia kuwa wamekutenga. Mimi nakuonea huruma sana. Ulikuwa umekaa vizuri kijijini, ukawa kipenzi cha kila mtu. Leo wanakutenga kwa ajili yangu. Mtu ambaye nimefika hapa kwa bahati mbaya.

Ambaye siwezi kukusaidia wewe kwa chochote. Mtu ambaye ni tegemezi kwako, kwani nimefika hapa nikiwa majeruhi, sina nguo, sina pesa."

"Sijui unaongea nini Bakari. Kwangu mimi ngumu zaidi ilikuwa ni kukusogelea wewe ukiwa umechakaa na sura yako kufunikwa na damu kwa ajili ya kipigo.

Nilikuwa sijui wewe ni nani. Ni majeruhi au tayari marehemu. Wenzangu wakaondoka, nikakumwagia maji kwa ajili ya kusafisha damu, ukaonyesha ishara ya kutaka maji ya kunywa, nikakunywesha. Ilikuwa ni jioni, saa 12:00, porini.

Pata picha mimi ni mtoto wa kike, nilifanya yote haya, nikijua ninalofanya inawezekana ikawa ni hatari kwa maisha yangu.

Leo eti wamenitenga, ndiyo niogope? Kama unataka kwenda nenda, lakini siyo iwe unaondoka kwa sababu yangu." Sauti ilikuwa ndogo, lakini yenye msisitizo iliyojaa kila aina ya ukweli na ushupavu wa kike.

"Najua kuwa unajiona kama mkosaji kwa sababu kama vile unaona nimekosa furaha ya kushirikiana na wenzangu kijijini kwa sababu yako. Ukweli ni kwamba mimi nafurahi zaidi navyozidi kukuweka hapa, mtu niliyekuokoa, nizidi kukuangalia hadi siku utakapoondoka.

Itakuwa ni kazi bure kufanya nilivyofanya, halafu nikwambie uondoke tu, bila kujua sasa unakwenda wapi, unaondoka vipi, na hao maadui zako, wako wapi, inawezekana wanakufuatilia."

Maneno hayo yalianza kumtoa machozi Bakari. Yalianza kutiririka. Siwatu aliacha kuongea anakabaki anamtazama.

"Sijawahi kuona mwanamke mwenye roho nzuri duniani kama wewe dada."

Siwatu alitabasamu, lakini alishindwa kusema chochote.




**"Haya bwana, tukimaliza kupalilia, kachimbe mihogo, mimi nachuma kisamvu na majani ya kunde kwa ajili ya chakula, si unajua tena haturusiwi kununua chochote dukani?"**

"Nitakapokwenda kwetu nitamwambia kila mtu habari juu yako. Sitoficha chochote"

"Usilie, kaka Bakari, jiandae tu twende shamba, ukanisaidie kuweka matuta shambani."

"Siyo kukusaidia. Mimi sina chochote cha kukulipa. Na hata kama nitalima kwenye mashamba yako mwaka mzima, sitoweza kulipa wema ulionifanyia.

Wema wako Siwatu ni wa asili, mimi wangu ni wa kuiga tu. Kwa sababu wewe ulinisaidia nikiwa nusu mfu, hukuhitaji chochote kutoka kwangu, lakini mimi chochote nitakachofanya kwako, ni kuiga tu ule wema ambao wewe umenifanyia. Vyote viwili ni wema. Lakini ni tofauti na hautolingana kamwe."

******************************

"Heheee hoiii, ni kwa kulazimisha hivyo. Yaani unalazimisha mwanaume kwa nguvu shoga. Hata hujui katoka wapi." Ilikuwa ni sauti ya kike ikisikika kutoka ndani ya nyumba moja.

Ilizungumzwa kwa namna ya mafumbo. Ni kama vile msichana huyo alikuwa akimwambia mwenzake. Lakini lilikuwa ni dongo kwa Siwatu.

Alikuwa anapita ameongozana na Bakari. Walikuwa wanaelekea shamba. Mashamba yake ya urithi na nyumba zake mbili ndiyo vitu pekee alivyotegemea Siwatu kuendesha maisha yake.

Hakuruhusiwa kununua chochote kwenye duka lolote. Hakusalimiwa wala kuitikiwa salamu na mtu yoyote. Ilikuwa ni utekelezaji wa kikao kilichokaliwa na kijiji.

"Chezea bwana wewe, bwana kutoka Msata." Sauti nyingine ya kike ilijibu.

Siwatu na Bakari waliangalia. Wakashangaana. Kwa sababu walikuwa wameshajua kila kitu kinachoendelea kijijini hapo haikuwapa shida. Wala mafumbo, kelele hazikuwafanya kuacha kile ambacho wao wamekipanga.

Kitu ambacho wengi walianza kuwa na wasiwasi nacho ni kwamba huenda kitendo cha Siwatu kugoma Bakari asiende kwao ni kwamba tayari alikuwa na uhusiano naye wa kimapenzi.

Kitendo cha Bakari kuhamia kwake ndiyo kabisa, wanakijiji wote wakapigia mstari. Usilolijua ni kama usiku wa kiza. Siwatu hakuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi na Bakari.

Walipendana kama binadamu waliosaidiana. Siwatu alimhifadhi kwa sababu ni mtu aliyemuokoa kutoka kwenye kifo, hivyo alitaka kuwa na muendelezo wa uhakika wa usalama wa aliyemsaidia mpaka atakapoondoka kwa hiari yake. Ndiyo maana aliamua awe naye karibu zaidi kutoka kwa watu wanaotaka aondoke.

Bakari alimpenda Siwatu kwa sababu ndiye mwokozi wake. Bila yeye saa hizi angekuwa ahera anapambana na maswali.

Pili ni kwamba ni yeye pekee kijijini hapo ndiye aliyejitolea kumtetea, kumlisha, kumlinda na kumhifadhi. Kwa maana hiyo ni lazima wawe wawili. Kuwa wawili kwa sababu ni mwanaume na mwanamke ikaonekana kama ni mtu na mpenzi wake.

"Hivi kwa nini hawa watu wanatuona kama mimi na wewe ni mtu na mpenzi wake?" Lilikuwa ni swali la kwanza alilouliza Siwatu baada ya kufika shambani.

"Kwa sababu tunaongozana popote tunapokwenda." Bakari alijibu kirahisi.

"Nadhani siyo hilo tu."

"Lingine lipi Siwatu?"

"Ujue kwa sababu tunalala wawili tu mle kwenye nyumba yangu, wewe mtoto wa kiume na mimi wa kike, basi wanajua haiwezekani, kuna kitu kinaendelea tu mle ndani."

"Wangejua kuwa mimi nalala chini wewe kitandani..." Kabla hajamaliza, Siwatu aliangua kicheko kilichomfanya apaliwe na kukohoa.

"Du pole sana dada."

"Ahsante, ila umenichekesha sana leo." Akajibu baada ya kikohozi kupungua.

"Kwani uongo?"

"Kweli, ila si nakwambia lala kitandani hutaki."

"Hapana, wewe ni dada yangu na mtu ninayekuheshimu sana kwenye maisha yangu."

"Kwani si unalala tu nimekwambia, kwani ukilala ndiyo huniheshimu?"

"Mmmh, sitaki mimi, huko kulalalala huko..." Kabla hajamaliza Siwatu aliangua tena kicheko.

"Leo mgeni umeamua kunivunja mbavu tu."

"Si tumetengwa bwana, bora tuvunjane tufurahi, tuchekeshane wenyewe kwa wenyewe."

"Haya bwana, tukimaliza kupalilia, kachimbe mihogo, mimi nachuma kisamvu na majani ya kunde kwa ajili ya chakula, si unajua tena haturusiwi kununua chochote dukani?"

"Sawa, ila usijali, kama kunatakiwa vitu muhimu kama mafuta, sabuni, dawa ya mswaki, sukari, mchele, unga, nitakwenda kununua kwenye vijiji jirani na hapa."

ITAENDELEA JUMAMOSI

# MICHUANO NGUMI RIDHAA KIMATAIFA MAMBO YAIVA

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kimataifa ya ngumi za ridhaa yanatarajiwa kufanyika kuanzia Mei 27 hadi 31, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Akizungumza jijini jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Shirikisho la Ngumi za Ridhaa Tanzania (OBFT), Mohamed Aboubakari, alisema lengo la mashindano hayo ni kuiandaa Timu ya Taifa ya Tanzania ambayo inatarajia kwenda kushiriki katika michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika baadaye mwaka huu.

Aboubakari alisema mabondia wa Tanzania wamefanya maandalizi ya muda mrefu na wanatarajia kupitia michuano hiyo watapata kikosi imara kitakachokwenda kupeperusha vyema bendera ya nchi.

"Maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na timu inaendelea kufanya mazoezi ili kuiweka miili sawa sawa, hatuna budi kuishukuru serikali yetu kwa kukubali kutupa ufadhili wa kuendesha mashindano," alisema Aboubakari.

Alizitaja nchi ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ni pamoja na Malawi, Sudani Kusini, Zambia, Kenya, Msumbiji, Zimbabwe na wenyeji Tanzania.

Aliongeza mabondia kutoka katika nchi hizo watanaanza kuwasili Tanzania kuanzia kesho tayari kushiriki michuano hiyo maalumu ya kuwaandaa.

"Mchakato wa kupima uzito wachezaji utafanyika siku hiyo hiyo ya mashindano asubuhi na jioni wataanza kupambana, tunaamini kila kitu kitakwenda vizuri na malengo yetu yatatimia," Aboubakari alisema.

Aliongeza kila timu itakuja na mabondia wanawake ambao wamealikwa kwa lengo la kuwapa nafasi ya kuonyesha uwezo wao na kujitangaza.

"Mashindano haya yatahudhuriwa na wadau mbalimbali wa mchezo huo, kwa maana hiyo yatawapa fursa mabondia wanawake kuonekana na, kwa upande wa Tanzania timu yetu ina wachezaji sita na inanolewa na Kocha Mkuu, Timoth Kingu," aliongeza kiongozi huyo.

Alisema pia wamezialika timu zote zilizo chini ya Jeshi la Magereza kwa lengo la kuangalia vipaji vya wachezaji ambao hapo baadaye wataitwa kwa ajili ya kushiriki mashindano mengine.

Michezo ya Jumuiya ya Madola inatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 28 hadi Agosti 8, mwaka huu katika mji wa Birmighan, Uingereza.



Winga wa KMC FC, Miraji Athuman (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya wachezaji wa Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. KMC ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Geita yaipigia hesabu Simba

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Geita Gold limesema linajipanga vizuri kuhakikisha wanapata matoke chanya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba watakayokutana nayo kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Minziro, alisema anatambua mchezo huo utakuwa mgumu na anaiheshimu Simba.

"Tunamheshimu mpinzani wetu, tunafahamu tunakutana na timu ambayo inafanya vizuri kwenye Ligi Kuu, hivyo tutaingia uwanjani kwa tahadhari," alisema Minziro.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na mazoezi na kila mmoja ana morali ya kukutana na mabingwa hao watetezi na kupata matokeo mazuri ili wajiimarishe katika msimamo wa ligi hiyo.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, George Ndiligenda alisema wamejipanga vyema kuondoka na pointi tatu muhimu za mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani.

"Mikakati yetu ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, tutahakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu yote iliyobakia," Ndiligenda alisema.

## Atlantic Mkwawa Rally kufanyika leo

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

MADEREVA 15 kutoka nchi mbalimbali wanatarajia kushiriki mbio za magari zijulikanazo kwa jina la Atlantic Mkwawa Rally 2022 zitakazofanyika kuanzia leo mkoani hapa, imefahamika.

Mbio hizo zimeandaliwa na Klabu ya Michezo ya Magari ya Iringa (IMSC) na kudhaminiwa na makampuni mbalimbali wakiwemo THAHI, Hoteli ya Iringa SunSet, AzamTV, Star Bull, Coca-Cola, Mount Royal Villa, Hope Service Station, Sign Express, KFC Ltd, Fleet Track na wadhamini wakuu ambao ni Atlantic Lubricants and Mkwawa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hidaya Kamanga alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na madereva wote waliothibitisha kushiriki kutoka Kenya, Zambia, Uganda na wenyeji Tanzania watashiriki ili kutimiza ndoto zao.

Naye Mwenyekiti wa IMSC, Amjad Khan alisema anaamini mashindano ya mwaka huu yatakuwa na ushindani zaidi kutokana na washiriki kufanya maandalizi ya muda mrefu.

Khan amewataka wananchi wa Iringa na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi leo na kesho kushuhudia madereva hao wanavyochuana katika mbio hizo ambazo hufanyika kila mwaka.

## Tax mgeni Lugalo Ladies Open 2022

**Na Cheji Bakari, TANGA**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Stergomera Tax anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mashindano ya gofu kwa wanawake yanayojulikana Lugalo Ladies Open yatakayofanyika leo jijini Dar es Salaam.

Mashindano hayo yatafanyika kwa siku mbili kwenye viwanja vya gofu Lugalo na maandalizi yake yamekamilika. Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Michael Luwongo, aliliambia gazeti hili mashindano hayo ya wanawake yana lengo la kuenzi siku ya Mama Duniani pamoja na kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii wa ndani na kukuza michezo.

Luwongo alisema wanawake wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano ya gofu ya kimataifa hivyo wanahitaji kuthamini michango yao.

"Wanawake wanafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na shindano hili la Lugalo Ladies Open 2022 ni maalumu kuenzi siku ya Mama Duniani, pia lina lengo la kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii wa ndani na kukuza michezo," alisisitiza Luwongo.

## ZISIKUPITE

### POGBA CITY KILIELEWEKA
PAUL Pogba alifikia makubaliano binafsi na Manchester City lakini amepinga hatua ya kuhama kutoka Manchester United kwa sababu kiungo huyo wa kati Mfaransa mwenye umri wa miaka 29 ambaye mkataba wake unaisha msimu huu, alikuwa anahofia kulaumiwa na mashabiki. ***(Times)***

### JUVE YAMTAKA POGBA
PAUL Pogba amebakia kuwa ndiye mchezaji anayelengwa na Juventus, ambao wana matumaini ya kumrejesha tena Mfaransa huyo Turin pamoja na kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 30 kutoka Chelsea. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MBAPPE KUFUNGUKA KESHO
NYOTA wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe atatangaza uamuzi wake kuhusu hali yake ya baadaye kesho, huku mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akihusishwa kwa muda mrefu na taarifa za kuhamia Real Madrid. ***(L'Equipe)***

### DEPAY AGOMBEWA EPL
KLABU za Arsenal, Newcastle na Everton zina nia na mshambuliaji wa Barcelona, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28. (Sport)

### DYBALA KUTUA SPURS
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala ameamua kuhamia Tottenham Hotspur huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 akisaka klabu atakayojiunga nayo siku zijazo baada ya kuthibitisha ataihama Juventus mwishoni mwa mkataba wake msimu huu. ***(AS)***

### LENGLET ANUKIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur pia ina nia ya kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Ufaransa, Clement Lenglet mwenye umri wa miaka 26 ambaye yuko tayari kuondoka Barcelona**.** ***(Sport)***

### LEWANDOWSKI KUTUA BARCA
KUHAMIA Barcelona ni kipaumbele kwa Robert Lewandowski wa Bayern Munich, huku mkataba wake utakaodumu hadi 2025 ukianza kujadiliwa, na mshambuliaji huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 33 bado hajazungumzia kuhusu hatima yake. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### DEST AKARIBIA UNITED
KLABU ya Manchester United imepewa ofa ya kumsajili beki wa Barcelona, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21. ***(90min)***

### MILAN YAMNASA ORIGI
DIVOCK Origi mwenye umri wa miaka 27 anatarajiwa kujiunga na AC Milan wakati mkataba wake na Liverpool utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

### HOURIHANE SOKONI
KLABU ya West Brom inataka kumsajili kiungo wa kati wa Jamuhuri ya Ireland mwenye umri wa miaka 31, Conor Hourihane, ambaye amekuwa akicheza kwa mkopo Sheffield United kutoka Aston Villa. ***(Football Insider)***

### ARSENAL KUMUUZA PEPE
KLABU ya Arsenal iko tayari kumuuza winga wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 26, Nicolas Pepe, ambaye walimsajili kwa ada ya pauni milioni 72 mwaka 2019. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAJIPANGA KUMSAJILI DEPAY

**Ni baada ya nyota huyo kutokuwa kwenye mipango ya kocha mpya...**

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal inawania kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Memphis Depay ili kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao, kwa mujibu wa Daily Mail.

Washikabunduki hao wanahitaji kuimarishwa safu yao ya ushambuliaji huku Alexandre Lacazette na Eddie Nketiah wote wakitarajiwa kuondoka msimu huu wa joto.

Depay alisajiliwa na Barca kwa uhamisho huru kutoka Lyon mwaka jana na amefunga mabao 13 kwenye mashindano yote msimu huu.

Lakini licha ya kuanza mechi nne zilizopita za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 28 amekuwa sio chaguo la kocha, Xavi.

Mkataba wake pale Camp Nou umebakia mwaka mmoja, ingawa kuna chaguo la kuongeza mwaka mmoja ikiwa klabu itaona inafaa.

Tarifa zaidi zinasema Everton na Newcastle pia wanawania kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United.

Katika miezi 18 aliyokaa Manchester United, Depay alifunga mabao mawili pekee katika mechi 33 akiwa na mashetani wekundu hao.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 200,

MECHI KALI
VALENCIA
VERSUS
CELTA VIGO
1 | 2.70
X | 3.25
2 | 2.55

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOULIBALY AZUNGUMZIA KUONDOKA NAPOLI




**NAPLES, Italia**

MLINZI wa Napoli, Kalidou Koulibaly amekata mzizi wa maneno kuhusu uhamisho wake wa kuondoka katika klabu hiyo na kusema ikiwa ataondoka basi itakuwa kwa sababu ya vipengele vya mkataba wake vimemruhusu.

Mchezaji huyo wa kimataifa kutoka Senegal amekuwa mmoja ya walinzi bora Ulaya huku akizivutia timu kadhaa kubwa na kuwafanya wahitaji huduma yake na mara kadhaa amehusishwa na kuondoka klabuni hapo.

Koulibaly aliambia Onze Mondial, "Sitakuwa sehemu ya mabishano kwa sababu ya kutaka kuondoka kwenye klabu. Ikiwa nitaondoka Napoli, itakuwa kwa sababu masharti ya mkataba yamenitaka kuondoka."

"Kutakuwa hakuna mabishano na nitakwenda kuzungumza na rais. Amejaribu kuwasikiliza mashabiki ambao hawataki mimi niondoke na kila muda amekuwa akiweka ada ya juu."

Koulibaly alijiunga na Napoli akitokea Genk mwaka 2014 na haikuchukua muda kujitengenezea ufalme kwenye nafasi ya ulinzi ndani ya Napoli na kuwa mmoja ya walinzi bora kwenye ligi tano bora Ulaya.

# Wan-Bissaka ruksa kuondoka United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imemruhusu Aaron Wan-Bissaka kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto kwa sababu beki huyo hatakuwa sehemu ya mipango ya kocha mpya, Erik ten Hag atakapoanza kazi hapo Old Trafford.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alimsajili Wan-Bissaka kutoka Crystal Palace mwaka 2019 kwa ada ya pauni milioni 50.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameshindwa kupata nafasi kwenye timu hiyo.

Wan-Bissaka ameshindwa kuonyesha kiwango chini ya Ralf Rangnick huku kocha huyo wa muda akimpa nafasi Diogo Dalot badala yake.

Mashetani Wekundu hao hao wangependelea mkataba wa kudumu kwa kinda huyo, lakini wapo tayari kwa kumuuza kwa mkataba wa mkopo iwapo una kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

Wan-Bissaka amecheza mechi 26 katika mashindano yote msimu huu na hajachangia vyema katika hesabu ya mabao ya United lakini amefunga bao la kujifunga.



,000,000

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/05/22 | 18:00 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.32 | 2.31 |
| 02. 22/05/22 | 18:00 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.42 | 2.87 |
| 03. 22/05/22 | 18:00 | Burnley vs Newcastle | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 04. 22/05/22 | 18:00 | Brighton vs West Ham | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 05. 22/05/22 | 18:00 | Brondby vs Silkeborg | 2.48 | 3.59 | 2.54 |
| 06. 22/05/22 | 18:30 | Kalmar vs Djurgardens IF | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 07. 22/05/22 | 18:30 | Elche vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.49 |
| 08. 22/05/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 09. 22/05/22 | 19:00 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 10. 22/05/22 | 21:00 | Ham-Kam vs Rosenborg | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 11. 22/05/22 | 23:00 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 12. 22/05/22 | 23:00 | Barcelona vs Villarreal | 2.47 | 3.60 | 2.58 |
| 13. 22/05/22 | 23:00 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.35 | 3.35 | 2.90 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 21/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3430 | Avispa Fukuoka vs Yokohama F Marinos | 3.30 | 3.25 | 2.04 |
| 14:00 | 3846 | Tom Tomsk vs Metalurg Lypetsk | 1.64 | 3.89 | 4.28 |
| 16:00 | 1175 | Altay vs Kasimpasa | 3.03 | 3.62 | 2.13 |
| 16:00 | 1528 | Kaizer Chiefs vs Moroka Swallows FC | 1.97 | 2.96 | 4.24 |
| 16:00 | 3591 | Bloemfontein Celtic vs Mamelodi Sundowns | 3.12 | 3.22 | 2.23 |
| 17:00 | 1066 | Nizhny Novgorod vs Zenit St Petersburg | 3.46 | 3.51 | 1.98 |
| 17:00 | 1463 | FK Khimki vs Spartak Moscow | 3.02 | 3.46 | 2.18 |
| 17:00 | 2292 | Rubin Kazan vs Ufa | 2.82 | 3.27 | 2.39 |
| 17:00 | 2786 | Sunderland vs Wycombe | 2.10 | 3.31 | 3.31 |
| 17:00 | 2857 | Rangers vs Hearts | 1.49 | 4.19 | 5.26 |
| 17:00 | 3728 | Arsenal Tula vs Ural Yekaterinburg | 4.14 | 3.55 | 1.80 |
| 17:00 | 4095 | FC Krasnodar vs Akhmat Grozny | 2.53 | 3.47 | 2.53 |
| 17:00 | 4492 | Sandefjord vs Lillestrom | 3.13 | 3.48 | 2.14 |
| 17:00 | 4835 | CSKA Moscow vs Rostov | 1.62 | 4.06 | 4.66 |
| 17:30 | 5968 | FC Eindhoven vs ADO Den Haag | 2.19 | 3.56 | 2.92 |
| 18:00 | 2192 | RB Salzburg vs Austria Klagenfurt | 1.06 | 9.16 | 20.45 |
| 18:00 | 2436 | Aarhus vs Nordsjalland | 2.38 | 3.73 | 2.58 |
| 18:00 | 3696 | Sonderjyske vs Viborg FF | 2.90 | 3.44 | 2.28 |
| 18:00 | 5885 | Austria Vienna vs Sturm Graz | 2.47 | 3.35 | 2.52 |
| 18:15 | 5464 | Genoa vs Bologna | 2.35 | 3.41 | 2.77 |
| 18:30 | 2022 | Helsingborg vs IFK Varnamo | 2.47 | 3.05 | 2.72 |
| 18:30 | 2880 | Legia Warszawa vs Cracovia | 1.81 | 3.36 | 3.99 |
| 18:30 | 3729 | Valencia vs Celta Vigo | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 19:00 | 3656 | Besiktas vs Konyaspor | 1.91 | 3.68 | 3.58 |
| 19:00 | 4548 | Molde vs Kristiansund | 1.34 | 5.35 | 7.13 |
| 19:00 | 5850 | Yeni Malatyaspor vs Fenerbahce | 9.95 | 6.37 | 1.22 |
| 19:30 | 3856 | Talaea El Gaish vs Arab Contractors | 2.34 | 2.74 | 3.54 |
| 20:00 | 1941 | Panathinaikos vs PAOK | 2.72 | 2.97 | 2.53 |
| 20:00 | 4023 | Barcelona W vs Lyon W | 1.46 | 4.29 | 5.46 |
| 21:00 | 2994 | SC Freiburg vs RB Leipzig | 3.64 | 3.44 | 2.02 |
| 21:00 | 3732 | Heracles Almelo vs SBV Excelsior | 1.81 | 3.77 | 3.82 |
| 21:00 | 3777 | Dinamo Zagreb vs Hajduk Split | 1.75 | 3.40 | 4.27 |
| 21:45 | 4194 | Atalanta vs Empoli | 1.21 | 6.73 | 9.70 |
| 21:45 | 4199 | Lazio vs Verona | 1.64 | 4.06 | 4.45 |
| 21:45 | 4406 | KAA Gent vs Charleroi | 1.63 | 4.18 | 4.48 |
| 21:45 | 4546 | Fiorentina vs Juventus | 1.94 | 3.67 | 3.42 |
| 21:45 | 5004 | Mechelen vs Racing Genk | 3.23 | 4.08 | 1.92 |
| 22:00 | 1180 | Nantes vs St Etienne | 2.54 | 3.48 | 2.54 |
| 22:00 | 2138 | Marseille vs Strasbourg | 2.10 | 3.49 | 3.19 |
| 22:00 | 3110 | Lens vs Monaco | 3.23 | 3.78 | 2.00 |
| 22:00 | 3255 | Angers vs Montpellier | 2.03 | 3.68 | 3.23 |
| 22:00 | 4870 | Lorient vs Troyes | 2.16 | 3.39 | 3.14 |
| 22:00 | 4981 | Clermont Foot vs Lyon | 3.68 | 3.98 | 1.81 |
| 22:00 | 5131 | Brest vs Bordeaux | 1.99 | 3.84 | 3.19 |
| 22:00 | 5199 | Lille vs Rennes | 3.99 | 3.89 | 1.76 |
| 22:00 | 5370 | Paris St Germain vs Metz | 1.20 | 6.89 | 10.60 |
| 22:00 | 5428 | Reims vs Nice | 3.83 | 3.73 | 1.83 |
| 22:00 | 5831 | GD Chaves vs Moreirense | 2.51 | 3.26 | 2.71 |
| 22:30 | 2891 | Columbus Crew vs Los Angeles FC | 2.36 | 3.38 | 2.93 |
| 23:00 | 1167 | DC United vs Toronto FC | 1.57 | 4.32 | 5.23 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA, YANGA ZAWEKEWA NGUMU KUMNASA MKANDALA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC umesema umefikia katika hatua nzuri ya mazungumzo ya kumbakisha klabuni hapo kiungo wake, Cleophace Mkandala ambaye anawaniwa na Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam.

Mkandala ameonyesha kiwango kizuri msimu huu na kuanza kuhusishwa na mipango ya kuondoka Dodoma Jiji FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dodoma jiji FC, Fortunatus Johnson alisema nyota huyo bado ana mkataba na timu hiyo ambayo unaisha Julai 30, mwaka huu na mazungumzo ya kumwongezea mkataba mpya yamefika hatua chanya.

Johnson alisema taarifa za nyota huyo kutakiwa katika klabu hizo anaziona katika mitandao, jambo ambalo wamelazimika kukutana na kiungo huyo kwa ajili ya kuwekana wazi na hatimaye kusaini mkataba mpya.

"Hatuna mpango wa kumwacha Mkandala, licha ya muda wa mkataba wake uliobakia unaruhusu kuzungumza na timu nyingine, hatuna hofu juu ya hilo kwa sababu tuko na mazungumzo mazuri na nyota huyo ya kuongeza mkataba mpya kusalia ndani ya Dodoma Jiji FC," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza klabu hiyo ina matumaini makubwa ya kumbakiza nyota huyo kwa sababu wana nafasi ya kuendelea katika mikiki mikiki ya ligi hiyo kwa msimu ujao.

"Mipango yetu kwa sasa ni kuhakikisha tunashinda michezo sita iliyosalia ili kujiweka katika katika nzuri ya kuendelea kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, tunaamini nafasi na uwezo wa kupambana tunao," Johnson alisema.

Naye Mkandala aliliambia gazeti hili kwa sasa hawezi kuzungumzia suala hilo kwa sababu anapigania timu yake kupata matokeo mazuri katika michezo iliyobakia ya msimu huu.

Mkandala alisema yeye bado ni mchezaji wa Dodoma Jiji na sasa nguvu na akili zake ziko katika kuhakikisha anasaidia timu yake hiyo kufikia malengo na kupata matokeo mazuri.

"Unajua sitaweza kusema lolote kwa sasa kuhusu mkataba wangu lakini nikuambie nguvu zangu ni kuhakikisha Dodoma Jiji inaendelea kubaki katika Ligi Kuu, baada ya hapo ndio nitaweka wazi juu ya hatima yangu kuendelea kutumikia Dodoma au kwenda kujaribu changamoto kwa timu ambayo itanihitaji," alisema Mkandala.



Makocha wa mpira wa miguu kwa timu za wanawake wakifuatilia kwa makini mafunzo maalumu yaliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Laliga yanayofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Yanga kubakiza vifaa vyake

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumwongeza mkataba wa miaka miwili kiungo mkabaji wake, Zawadi Mauya, Yanga imesema itaendelea na mchakato huo hadi pale watakapomaliza wachezaji wote ambao wanawahitaji kubaki kwa ajili ya msimu ujao.

Juzi jioni Yanga ilitangaza rasmi imempa mkataba mpya kiungo huyo aliyesajiliwa akitokea Kagera Sugar baada ya mkataba wake wa awali kuelekea ukingoni.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wataendelea kuwasajili na kuwatambulisha mmoja mmoja hadi pale watakapomaliza wachezaji wote ambao wamependekezwa kubaki na benchi la ufundi.

"Tunaendelea mmoja baada ya mwingine, wataendelea kutangaza, nyinyi tulieni tu. Wale ambao bado sisi tunawahitaji hawatoondoka," alitamba Bumbuli.

Kwa siku chache zilizopita, Yanga imekuwa ikiwaongeza mikataba wachezaji wake muhimu ndani ya kikosi hicho.

"Najisikia furaha nimebaki Yanga kuitumikia timu yangu, nashukuru kwa wananchi kuendelea kuniamini, nyinyi mmetaka kama wanachama na mashabiki, mimi nani nisiweze kukubali kuendelea. Ahsanteni wananchi na wanachama, mimi Zawadi Mauya, bado nipo nipo sana," alisema mchezaji huyo baada ya kukamilisha usajili wake. Nyota wengine ambayo Yanga imewapa mikataba mipya ni pamoja na Bakari Mwamnyeto na Kibwana Shomari.

# Michezo

Jumamosi Mei 21, 2022

Nipashe







Arsenal yajipanga kumsajili Depay




Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola (katikati), akifafanua jambo mbele ya makocha wenzake wakati wa mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kocha Mkuu, Pablo Franco. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YAPANGUA KIKOSI CHA YANGA

●●●Nabi alazimika kubadili mfumo wakati Barbara, Manara kikaangoni TFF...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

ILI kuhakikisha wanafikia malengo yao msimu huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amepanga kupumzisha baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza katika mechi dhidi ya Biashara United kwa ajili ya kuwaweka fiti kuelekea mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba utakaochezwa Mei 28, mwaka huu.

Yanga itakutana na Biashara United keshokutwa ikiwa ni siku tano zimebakia kabla ya kuvaana na Simba kwenye dimba la CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anahitaji kuwapa mapumziko baadhi ya wachezaji wake kwa ajili ya kuwaandaa kisaikolojia na mchezo huo ambao hawahitaji kupoteza.

Nabi alisema uamuzi wa kufanya mabadiliko katika mchezo dhidi ya Biashara United unalenga kuongeza nguvu ya kuwakabili Simba na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo ambayo watani zao pia wanaushikilia ubingwa.

"Ni mechi ngumu na yenye presha kubwa kwa sababu tayari tumekuwa na asilimia kubwa ya kutwaa ubingwa wa ligi lakini pia bado tunahitaji taji la Kombe la FA, lazima tushinde dhidi ya Simba ili tucheze fainali," alisema Nabi.

Aliongeza wanahitaji kutafuta matokeo mazuri katika michezo yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia pamoja na kushinda mechi dhidi ya Simba na ili wafikie malengo, analazimika kupangua kikosi chake.

"Huu wakati nalazimika kuwatumia wachezaji wote waliopo ndani ya kikosi changu na kwa wale walitumika sana wanahitaji kupumzika," Nabi alifafanua.

Alisema bado wachezaji wake wanatakiwa kupambana katika kila mechi wanayocheza kwa sababu bado hawajamaliza kazi na hawajafikia malengo waliyonayo ya msimu huu unaoelekea ukingoni.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez pamoja na Msemaji wa Yanga, Haji Manara wameitwa katika Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutokana na malalamiko yaliyofikishwa kwenye kamati hiyo.

Barabara amefikishwa katika kamati hiyo akilalamikiwa na Yanga kwamba kupitia redio moja ya Afrika Kusini alitoa shutuma zisizo za kweli dhidi ya klabu hiyo ambayo kwa sasa inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga ilidai kauli iliyotolewa na Barbara inachafua taswira ya klabu yao mbele ya umma, hivyo wanaitaka kamati hiyo imchukulie hatua.

Simba nayo iliwasilisha malalamiko yake dhidi ya Manara ikidai kupitia mtandao wa kijamii, ofisa huyo alitoa shutuma zisizo za kweli dhidi ya klabu yao, jambo ambalo ni kukiuka Kanuni za Maadili za TFF, Toleo la mwaka 2013.

Tayari Kamati ya Maadili ilishawasilisha mashtaka kwa walalamikiwa hao pamoja na wito wa kuhudhuria mashauri hayo ambayo yalianza kusikilizwa tangu Mei 14, mwaka huu.

"Kikao cha kesho (leo), ni mwendelezo wa Kamati ya Maadili ya TFF katika kusikiliza mashauri hayo," ilisema sehemu ya taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo.

Simba na Yanga zimekuwa zikituhumiana kila upande unafanya vitendo vya hujuma kwa mwenzake zinapokuwa na mechi za ndani pamoja na zile za kimataifa kwa lengo la kutaka kuona hazipati matokeo chanya.

Kwa sasa Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara lakini Simba iliyoko nafasi ya pili inashikilia ubingwa huo kwa misimu minne mfululizo, imefika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya CAF mara tatu katika miaka ya karibuni lakini pia inashikilia Kombe la FA kwa misimu miwili mfululizo.

## Stars kuifuata Niger 'kibishi'

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuanza kuonyesha makali katika mechi mbili zilizopita, nahodha wa Simba, John Bocco ameendelea kuachwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa na michezo ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) zitakazofanyika nchini Ivory Coast.

Stars itaingia kambini Mei 28, mwaka huu kwa ajili ya kuikabili ugenini Niger , hapo Juni 4 na Juni 8, mwaka huu watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuwakaribisha Algeria.

Kikosi kamili cha Taifa Stars kilichoitwa kwa ajili ya mechi hizo mbili ni makipa watatu, Aishi Manula kutoka Simba, Metacha Mnata (Polisi Tanzania) na Abutwalib Mshery wa Yanga huku mabeki ni Shomari Kapombe, Mohammed Hussein, Kennedy Juma, Mzamiru Yassin na Kibu Denis wote kutoka Simba.

Nyota wa Yanga walioitwa Stars ni Kibwana Shomari, Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Feisal Salum 'Feisali Toto', Salum Abubakar 'Sure Boy' na Farid Mussa.

Wachezaji wengine ni Haji Nonga (Weymouth – Uingereza), Abdallah Kheri (Azam FC), Nickson Kibabage (KMC), Himid Mao (Ghazl El Mahalla ya Misri), Novatus Dismas (Beita Tel Aviv Balyan ya Israel), Aziz Andabwile (Mbeya City), Simon Msuva (huru), Ben Starkie (Spalding, England) Abdul Suleiman (Coastal Union), Reliants Lusajo (Namungo FC), George Mpole (Geita Gold FC) na Ibrahim Koshua (Tusker Kenya).

Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Shadrack Nsajigwa alisema kutokana na kukosa muda, timu hiyo haitacheza mchezo wa kirafiki kabla ya kuwavaa Niger.

Nsajigwa alisema pia licha ya kukosa timu, wameamua kumuita Msuva kwa sababu wana imani ataisaidia Stars kama alivyofanya katika mechi iliyopita hali ya kuwa hakuna na klabu ya kuitumikia.

"Tumemuita kwa sababu ana mchango mkubwa ndani ya timu yetu ya taifa, pia itamsaidia kuonekana na kupata timu nje ya nchi," alisema Nsajigwa.

Naye Kocha wa Makipa wa timu hiyo, Ivo Mapunda alisema wamemuita Mshery kwa ajili ya kumwandaa ingawa anaamini ana uwezo mkubwa wa kucheza endapo atapata nafasi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >